# Nipashe

Jumatatu Juni 29, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580270

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN

215779502




## JPM atumbua DAS mkutanoni, ateua mrithi wake hapo hapo

UKURASA 3

### URAIS ZANZIBAR

# Maalim Seif ataja sababu tano kugombea mara ya 6

- Asema hana imani na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, atasimamia na kulinda ushindi... *Endelea Uk. 2*

### BAA LA CORONA



Tahadhari bado zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya ugonjwa wa corona, ingawa katika baadhi ya nchi kunaonekana maambukizi ya ugonjwa huo kupungua. Watu wanashauriwa kuendelea kufuata mwongozo wa kujilinda na si kupuuzia kwa kuwa ugonjwa bado upo. WHO

- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (katikati), akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Kulia ni Mwenyekiti wa Mkutano huo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Dk. Ally Laay na Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki hiyo, Fredrick Nshekanabo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## POLISI YAPIGA KAMBI GAIRO KISA WALIMU KUCHOMWA MISHALE

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Kilichowabeba mawaziri vijana wa Rais Magufuli

UK. 4

MICHEZO SIMBA BINGWA RASMI 2019/20 UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Maalim Seif ataja sababu kugombea urais Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KWA mara nyingine Maalim Seif Sharif Hamad ametangaza nia ya kugombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Act-Wazalendo ikiwa ni mara ya sita kugombea nafasi hiyo toka mwaka 1995.

Akizunguma na waandishi wa habari jana Mjini Zanzibar, alisema amefikia uamuzi huo kutokana na sababu tano zilizomsukuma ikiwamo kutoridhishwa na jinsi nchi inavyoendeshwa.

Alisema hivi sasa mfumo wa vyama vingi upo hatarini kutoweka kutokana na Watanzania kuamua kwa makusudi kuvunja misingi ya demokrasia.

"Kwa kuzingatia hatari hii nimeona ni hekima kukubali ushauri wa watu wengi kwamba huu si wakati wa kuacha mapambano bali ninawajibu kushirikiana na viongozi na vijana kuwavusha katika wakati huu mgumu katika historia ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Alitaja sababu nyingine kuwa mwaka 1992 yeye na wenzake waliamua kuanzisha Chama cha CUF na kuwashawishi wananchi kukiunga mkono ambacho kilikuwa na malengo ya wazi ya kurejesha haki bila ya ubaguzi, kupinga ukandamizaji na nchi kukwama.

Alisema hali hiyo ilikuwa ni mwiba kwa watawala wasiopenda kuiona Zanzibar ikikwamuka kimaendeleo na ndipo wakaamua kutumia dola kukidhoofisha chama hicho na hatimaye kufukuzwa kwenye chama kinyume cha matakwa ya wanachama.

Alieleza kuwa yeye ni nahodha mzoefu kwa kuliongoza jahazi, hivyo amekubali kuliongoza jahazi la kuleta mabadiliko kupitia ACT-Wazalendo.

"Katika hali hii nimeona haitokuwa busara ikiwa nahodha mzoefu wa kuongoza watu kuingia katika jahazi jipya halafu kuwaacha mkondoni...nimekubali ushauri kuwa niongoze juhudi za kuleta mabadiliko kupitia ACT -Wazalendo hasa wakati huu nchi yetu inapoelekea kuandika historia mpya," alisema.

Maalim Seif alisema jahazi jipya linahitaji nahodha mwenye uzoefu mkubwa aweze kuivusha Zanzibar kupisha dhoruba kali na yenye mawimbi mazito yanayoikabili.

Alieleza kuwa viongozi na wanachama wa chama hicho wamemwamini kupeperusha bendera ya kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar.

Alisema ameona si uungwana hata kidogo kudharau imani hiyo na badala yake anapaswa kuheshimu kwa kuwaongoza Wazanzibari kufikia ndoto ya Zanzibar wanayoitaka.

Aidha, Maalim Seif alisema licha ya sababu hizo alikaa na kujiuliza swali je, bado Wazanzibari wana hamu na yeye na ndipo alipotuma wataalamu kufanya utafiti, lakini matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuwa imani ya Wazanzibari kwake haijashuka hata kidogo.

"Inasikitisha na kuniumiza sana kwa kazi nzuri tuliyoifanya mimi na Rais mstaafu Amani Karume kwa kusaidiwa na kati ya maridhiano kwa kuwaunganisha Wazanzibari, lakini leo hii Wazanzibari wamegawiwa kwa sababu ya ubaguzi," alidai.

Maalim Seif alisema kuwa Julai 4 mwaka huu atachukua fomu ya kugombea nafasi ya urais na kuendelea na kauli yake ya kuwa hana imani na Tume ya Uchaguzi lakini wanajipanga na kujitayarisha kulinda ushindi wao kwa hali yoyote.

Kwa kipindi chote ambacho Maalum Seif alichogombea kura hazikutosha, na kwa mara ya kwanza alipata kura asilimia 49.76 na mshindi kuwa Salimin Amour aliyepata asilimia 50.24.

Mwaka 2000 alipata kura asilimia 32.96 dhidi ya asilimia 67.04 alizopata Amani Karume. Mwaka 2005 aligombea tena na kupata asilimia 46.07 huku Karume kiibuka mshindi kwa asilimia 53.18.

Mwaka 2010 alipata kura asilimia 49.1 huku Dk. Ali Mohamed Shein 2015 matokeo yalifutwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na Mwenyekiti wake, Jecha Salum Jecha, na yalitangazwa marudio Machi 20, mwaka 2016.




Amiri Mkuu wa Taasisi za Kiislamu Tanzania, Shekh Mussa Kundecha (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Baraza la Dini Mbalimbali (IRCPT) kutoa mwongozo wa mafunzo ya ujenzi wa amani kwa jamii kuendeleza uhusiano kati ya jamii na nchi. Kushoto ni Imamu wa Msikiti wa Rahmani ulipo Kimara, Shekh Rajabu Msinde na Mjumbe wa Baraza la Waislamu Wilaya ya Kinondoni, Abdul Magomba. **PICHA NA JUMANNE JUMA**.

# WALIMU KUPIGWA MISHALE

## Polisi Morogoro yapiga kambi Gairo

**Na Idda Mushi,** GAIRO

SIKU chache baada ya gazeti hili kuripoti kwa kina tukio la walimu wa Shule ya Sekondari Iyongwe, wilayani Gairo mkoani Morogoro, kushambuliwa kwa mikuki na watu wasiojulikana, Jeshi la Polisi limechukua hatua.

Hatua zilizochukuliwa na jeshi hilo mkoani humo ni kuweka kikosi kazi maalum kikiongozwa na Mkuu wa Upelelezi Mkoa, Kamishna Msaidizi wa Polisi Robert Mlasani na Ofisi ya Mkuu wa Polisi Wilaya ya Gairo.

Vigogo hao watapiga kambi katika Kijiji cha Chihwaga ilipo shule hiyo ili kuwasaka wote waliohusika na matukio hayo na kuwachukulia hatua za kisheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Mutafungwa, juzi alikatiza ziara ya kikazi wilaya za Malinyi, Kilombero na Ulanga, na kuelekea Gairo baada ya habari hiyo kuandikwa kwa kina.

Akiwa kijijini humo, aliwataka raia wema, wanaopenda elimu na maendeleo ya kijiji hicho kusaidia kuwafichua watu waliohusika na mauaji ya Mwalimu Madaraka Manilwa yaliyotoka Februari 24, mwaka huu na mwingine Hosea Charles akijeruhiwa kwa mkuki Juni 20, mwaka huu.

"Angalieni hapa Mkuu wa Shule (mwalimu Maria Mdoe) yuko peke yake kwenye huu mkutano, yuko wapi mwalimu Madaraka (aliyeuawa), yuko wapi mwalimu Charles (aliyejeruhiwa), wako wapi walimu wengine wa Iyogwe, hawa wote hawapo kutokana na vitendo vya baadhi yenu, watoto wenu, ndugu zenu wanaohusika na matukio haya ya kinyama," alisema Kamanda Mutafungwa.

Kamanda huyo alifanya mkutano mahali palipotokea tukio hilo katika uwanja wa Shule ya Sekondari Iyongwe.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, watakaoficha taarifa za matukio hayo kwa kukaa kimya wataunganishwa kwenye matukio hayo kama wahalifu, huku akitaka wenyeviti wa vijiji kukaa na wananchi wao na kuweka mikakati kuhakikisha matukio hayo hayajirudii.

Aidha, aliwataka kuanzisha vikundi vya ulinzi na usalama kulinda pamoja na mambo mengine mali na majengo ya serikali pamoja na watumishi kwa kufanya doria zenye tija kwani walimu wasipofundisha, watoto hawatasoma na kuzalisha lindi la umaskini katika maeneo hayo.

Kamanda huyo alisema kikosi kazi hicho kitafanya kazi usiku na mchana kuwabaini watuhumiwa wote wa matukio hayo ya kuua na kujeruhi, ingawa kesi ya mauaji tayari iko kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Morogoro ikiwahusisha watuhumiwa wawili walioko mahabusu na wengine walitoroka wakiendelea kusakwa.

"Tukio la kwanza la mauaji ya mwalimu Madaraka lilitushtua sana, baada ya watu kumvamia, akapambana nao na walipoona anawashinda, wakamchoma mkuki shingoni na kupoteza maisha akiwa njiani kupelekwa hospitali," alisema.

Aidha, alitoa siku mbili kwa wananchi wenye mikuki na mishale yenye sumu, au sumu ikiwamo ya mamba kwa ajili ya mikuki hiyo kusalimisha kwa hiari kwa wenyeviti wa vijiji kabla msako mkali haujaanza kuwabaini.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Iyongwe, aliimba serikali kulishughulikia suala hilo kwa kina ili kurejesha hali ya utulivu kwa walimu.

**VYOMBO VYA HABARI IPP VYASIFIWA**

"Ninavishukuru vyombo vya habari vya IPP, kazi mliyoifanya ni kubwa sana, mmejitoa sana kwenye jambo hili na Mungu awabariki nyote, mmefanya kila mtu akajua kinachoendelea, naishukuru pia serikali, na Jeshi la Polisi, wametukimbilia na wamechukua hatua kubwa kukabiliana na hili," alisema Mdoe.

Baadhi ya wananchi George Simion mkazi wa kijiji cha Makuyu na Charles Joctan Lwanda wa kitongoji cha Lebenya, waliomba usalimishaji wa mishale na mikuki yenye sumu na sumu yenyewe, kulenga wanaotumia vibaya silaha hizo kwa vile ni za kijadi na zimetumika toka enzi ya mkoloni kwa uaminifu mkubwa.

Walisema uwapo wake haukulenga kuwadhuru binadamu, hivyo wenye akili timamu na wasio na historia ya uhalifu waachwe kumiliki.

Naye, Askofu Samuel Elieza Kisigila, Katibu wa Jukwaa la Amani katika Wilaya ya Gairo na Charles Lwanda, waliomba kujengewa kituo cha polisi kutokana na wananchi wa maeneo hayo kulazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 45 kufuata huduma za Polisi Gairo Mjini.

Ombi lililokubaliwa na Kamanda huyo kwa kumwagiza OCD wa Gairo, SP Julieth Lyimo, kuwasiliana na viongozi wa vijiji ili kuona uwezekano wa kupata maeneo yasiyo na migogoro na watatoa ramani kazi hiyo ianzishwe na wananchi wenyewe na Polisi watawapatia askari.

Wananchi wengine Francis Meshack, Penina Mwangalimi na Happyness Mwangalimi walisema hawaridhiki na kitendo cha walimu kutaka kuwakimbia na kudai wameumizwa sana kwa matendo yanayoendelea.

HABARI KITAIFA

# JPM atumbua DAS mkutanoni

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli jana alitengua uteuzi wa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kisarawe, Mtela Mwampamba, na kumteua mwingine papo hapo ambaye alikuwa Ofisa Tawala na kumpa kiti meza kuu.

Alimteua Mwanana Msumi na kuagiza aandikiwe barua ya uteuzi jana hiyo na kuagiza aliyetenguliwa kutafutiwa nafasi ya chini anayoiweza nje ya wilaya hiyo.

Rais alifikia uamuzi huo jana wakati akiwa mkoani Pwani kwenye uzinduzi wa mradi wa maji kutoka Kibamba hadi Kisarawe.

Kabla ya kutangaza uamuzi huo, alisema kuwa DAS huyo ana tuhuma za kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wake za watu.

"Lakini hapa kuna tatizo la mteule wangu mmoja DAS, ninaambiwa ana mambo ambayo hayaendani na maadili ya kazi yake. Zipo tuhuma kwamba anachukua hata wake wa watu," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Nilikwisha kumwonya siku za nyuma nafikiri hakuweza kuonyeka na kwa sababu jukumu langu pia ni kusimamia maadili na nidhamu za watendaji, ninakuagiza Jafo (Waziri wa TAMISEMI) uongee na George Mkuchika (Waziri wa Nchi, Ofisi ya

Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwamba huyu kazi ya U-DAS nimeitengua leo, mtafutieni kazi ya chini aliyo na uwezo nayo na asifanye hapa."

"Kwa hiyo utamweleza Mkuchika aniletee mapendekezo au kama yuko hapa ambaye mnamuona anafaa U-DAS tumpe, tumalize hapa hapa kwani lazima tusibiri?" Aliuliza Rais Magufuli.

Rais Magufuli aliuliza kama kuna mwenye sifa anayefaa kushika nafasi hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, alisimama na kumpendekeza Msumi ambaye alipoulizwa elimu yake alisema ana shahada ya uzamili ya Utawala wa Umma.

Baada ya ofisa huyo kujitambulisha, Rais Magufuli alimteua hapo hapo na kumwambia apande jukwaa kuu kuketi kwenye meza kuu.

"Rais hapa kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuna Ofisa Tawala ambaye anaweza kabisa kufanya kazi hiyo," alisema Mkuu wa Mkoa huo wa Pwani.

"Kuanzia leo utakuwa DAS ili na ninyi mkagombanie wanaume na Mkuu wa Wilaya ili wote mwondoke...mwandikieni barua leo aipate, huyu ndiye DAS wa Kisarawe," aligiza Rais Magufuli.

"Lakini pia napenda kumpongeza Jafo kwa kunisaidia kazi akiwa Waziri wa TAMISEMI. Kijana huyu anajituma sana, mwembamba kwa umbo, lakini mambo yake makubwa, anazunguka kila mahali, sijasema mawaziri wengine hawafanyi kazi, lakini niko kwenye Jimbo la Kisarawe ni lazima nimsifie amejitahidi kwa kiasi chake," alisema Rais Magufuli.

"Amenisaidia sana na ndiyo maana mtaona katika miradi mbalimbali ya vituo vya afya, barabara na katika vitu vingine amekuwa akifuatilia, kwa hiyo nitashangaa sana wana Kisarawe kama haya ambayo ameyafanya Jaffo hamkuyaona, lakini mwenye macho haambiwi tazama."

Aidha, alimpongeza pia Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, kwa kufanikiwa kuondoa ziro katika wilaya hiyo.

**MRADI WA SGR**

Rais Magufuli akizungumza baada ya kutembelea mradi wa reli ya kisasa, alisema amerídhishwa na kasi ya ujenzi wake na kuwaomba makandarasi kuhakikisha unamalizika kwa wakati uliopangwa au ikiwezekana kabla ya wakati huo.

"Nawapongeza makandarasi wanafanya kazi nzuri nimeona 'structure' (muundo), mambo ni mazuri, nataka niwahakikishe wanamaliza mapema, mradi huu unagharimu zaidi ya Sh. trilioni 7.026 zimetolewa na Watanzania, tunahitaji treni ya namna hii iwe hapa kama Ulaya," alisema Rais Magufuli.

"Nataka siku moja mtu akiteremka Tanzania ajue ni Ulaya, nataka kuwahakikishia Tanzania mpya inakuja, inawezekana kwamba watu wanadhani kwamba ninaota ila mimi huwa sioti mchana, ninaota usiku."

**HARAMBEE UJENZI WA SHULE**

Rais Magufuli akiwa katika ziara yake, alisimama mara kadhaa kusikiliza kero za wananchi na katika Kijiji cha Soga alikutana na kero ya miundombinu mibovu ya shule ya msingi, na kuendesha harambee ya kuchangia ujezi wa shule hiyo na kufanikiwa kukusanya Sh. 68,535,000 huku akichangia Sh. milioni 5.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tanga, Yosepher Komba, akizungumza juzi na washiriki wa semina maalum kwa wasichana mkoani Tanga iliyoandaliwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Wanawake na Uongozi. **PICHA: OSCAR KASIMIRI**

# James Mbatia: Hakuna chama kiranja wa vingine

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, amesema hakuna chama cha siasa ambacho ni kiranja kwa mwenzake, huku akivitaka vyama katika uchaguzi mkuu kushindana kwa hoja.

Sambamba na hilo, ameitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhakikisha haki inatendeka kwenye uchaguzi huo kwa kusimamia sheria na kuwaondoa wale wote wanaotaka kuitia doa Tume hiyo.

Kauli hiyo aliitoa wakati akizungumza na watiania 113 wa nafasi za ubunge kupitia chama hicho Tanzania Bara.

Alisema chama hicho ni cha kuunganisha Taifa na sio cha mkoa mmoja na kabila moja, hivyo kwenye uchaguzi vyama vishindane kwa hoja za msingi na si kwa propaganda.

"Wale wanaosema NCCR kinataka kufungua NGO ni ndoto za alinacha sisi upole wetu sio dhaifu...Na sio vyama vingine vitake tufuate mbinu zao, hakuna chama ambacho ni kiranja wa mwenzake hapa hakipo," alisema.

Mbatia aliongeza: "Mbona kuna watu wengi waliondoka NCCR hatukulalamika na tuliwatakia kila la kheri wengine sasa wamerudi kwenye asili yao imeibuka minong'ono, hapa ndio asili ya mageuzi ya nchi, uwezo huo tunao na twende kifua mbele kwa kujiamini na tunaweza."

Mbatia alisema katika uchaguzi Tume ihakikishe haki sawa inatendeka katika kampeni na uchaguzi.

"Kwenye kura tupigiwe kura sisi halafu tutulie tuseme sisi ni watu wa utu hiyo hapana, yaani nione Selasini amepigiwa kura Rombo ameshinda, haki yetu lazima tuitafute kwa gharama yoyote lakini gharama ya amani, maelewano, sheria na kuifanya Tanzania kuwa sehemu salama ya kuishi," alisema.

Aliviomba vyama vingine kutambua kuwa mambo ya uchaguzi ni shirikishi na kuvumiliana kwa kuwa na fikra tofauti.

"Itikadi yetu ni kati ya itikadi bora duniani, sisi tutahubiri yaliyomema, Watanzania tunaomba wachague madiwani, wawakilishi, wabunge wa Nccr Mageuzi," alisema.

Kadhalika, alisema chama hicho kinaamini haki ya mtu binafsi kugombea.

Alisema kwa kuchagua wabunge na madiwani wa chama hicho ana uhakika kilio chao cha kupata Katiba mpya kitasikilizwa.


IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 38 2020

In the Matter of the Estate of the late JOSIA ANDREA CHIPANGA of Mohamanyika Area within Dodoma Region

AND IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY KENNEDY JOSIA ANDREA

GENERAL CITATION
(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 29 Day of June 2020.
Date at Dodoma this 28th day of May 2020.

PETITIONER
Presented for filling this 29th day of May 2020

RESIDENT MAGISTRATE

115792002



JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
16/06/2020

TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe 30/06/2020 kampuni ya c**hico (china henan internation cooperation group co.ltd)** itasafirisha mzigo **(Machine EXCAVATOR)** wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DODOMA** kuelekea **TABORA kupitia ITIGI** , gari hilo lenye namba za usajiri **T346 BDU / T888 BDT ,yenye escort no T645 CVZ**
2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo
   **Urefu - mita 20.00m**
   **Upana - mita 3.00m**
   **Kimo - mita 4.5m**
3. Njia itakayo tumika ni **DODOMA hadi TABORA kupitia ITIGI** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu*

115792102



JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
16/06/2020

TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe 27/06/2020 kampuni ya **chico (china henan internation cooperation group co.ltd )** itasafirisha mzigo (4 modle pipe) wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TABORA** kuelekea **DODOMA** kupitia **ITIGI** , gari hilo lenye namba za usajiri **T346 BDU / T888 BDT,yenye escort no T645 CVZ**
2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo
   **Urefu - mita 20.00m**
   **Upana - mita 3.00m**
   **Kimo - mita 4.5m**
3. Njia itakayo tumika ni **TABORA** hadi **DODOMA kupitia ITIGI** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu*

115792102

# Kilichowabeba mawaziri vijana

Na Mwandishi Wetu

RAIS John Magufuli mara kadhaa alifanya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri hadi anamaliza na mawaziri sita kati ya alioanza nao, huku kukiwa na vijana ambao wamefanya vizuri kwenye sekta zao.

Aidha, wapo waliaonza kama Manaibu Waziri na kupewa uwaziri kamili na wengine kuingia katikati ya safari na kufanya mambo makubwa katika nafasi zao kiasi cha kugusa moyo wa rais na kuwasifia hadharani.

**DOTTO BITEKO**



Dotto Biteko ni waziri kijana ambaye alitumikia nafasi yake kwa umahiri mkubwa ambaye kitaaluma ni mwalimu na aliingia katika Baraza la Mawaziri, Januari 9, mwaka 2019 akichukua nafasi ya Angela Kairuki ambaye alikuwa Waziri anayeshughulikia Uwekezaji.

Biteko ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Bukombe mkoani Geita, Januari 6, 2018 aliteuliwa na Rais Magufuli kuwa Naibu Waziri wa Madini nafasi ambayo aliitumikia kabla ya kupanda na kuwa waziri kamili.

Akivunja Bunge la 11, Rais Magufuli alisema kutokana na mapinduzi mbalimbali yaliyofanyika, kwa sasa sekta ya madini imeanza kukua kwa kasi, ambapo mwaka 2019 iliongoza kwa ukuaji (kwa asilimia 17.7), ikifuatiwa na ujenzi asilimia 14.1.

Alisema mapato yatokanayo na madini yameongezeka, ambapo mwaka 2018/19 zilikusanywa Sh. bilioni 346 kutoka Sh. bilioni 194 mwaka 2016/2017.

Mwaka 2019/2020 serikali inatarajia kukusanya Sh. bilioni 470, na kwamba Aprili 2020 pekee, licha ya kuwapo kwa tatizo la ugonjwa wa corona, imekusanya Sh. bilioni 58.

Mafanikio chini ya uongozi wake ni uanzishwaji wa Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited ambayo iliingia ubia na Kampuni ya Barrick Gold Corporation na kuanzisha Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited.

Kutokana na uwekezaji huo, serikali inamiliki hisa asilimia 16 na Kampuni ya Barrick Gold Corporation inamiliki hisa kwa asimilia 84, na kutakuwa na mgawanyo wa manufaa ya kiuchumi ya 50:50.

Mafanikio mengine ni uanzishwaji wa masoko na vituo vya ununuzi wa madini katika maeneo mbalimbali yenye shughuli za uchimbaji madini nchini, ambayo yamesaidia kutatua changamoto za muda mrefu za sekta ya madini husasan wachimbaji wadogo kukosa masoko ya uhakika na bei stahiki.

Mathalani, katika kipindi cha kuanzia Machi 2019 hadi Februari 2020 kupitia masoko wachimbaji wadogo wamefanya biashara ya madini yenye thamani ya Sh. 1,088,693,000,153.19 na kuingiza serikali mapato kwa kulipa mrabaha na ada ya ukaguzi wa Sh. 78,008,413,233.13.

Masoko haya yameleta mabadiliko katika Sekta ya Madini ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa sekta hii kwa kipindi cha Januari hadi Septemba iliongezeka kutoka asilimia 0.9 mwaka 2018 hadi asilimia 12.6 mwaka 2019 kwa kipindi kama hicho.

Mafanikio mengine ni uanzishwaji wa eneo Tengefu la Mirerani na kukamilisha ujenzi wa ukuta kuzunguka machimbo ya madini eneo hilo na kuweka vifaa vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha kuwa madini ya Tanzanite ambayo ni rasilimali ipatikanayo Tanzania pekee inalindwa.

Kutokana na mabadiliko hayo mapato ya wachimbaji wadogo yameongezea mara dufu kutoka Sh. 166,094,043 kabla ya kujenga ukuta hadi Sh. 2,150,000,000 baada ya kujengwa kwa ukuta.

Hivi karibuni, serikali ilinunua jiwe la tanzanite kutoka kwa mchimbaji, Saniniu Laizer, ikiwa jiwe moja lenye kilo 9.2 kwa thamani ya Sh. bilioni 4.5 na la pili lenye kilo 5.8 lenye thamani ya Sh. bilioni 3.3 na kumfanya kupata jumla ya Sh. bilioni 7.8.

Tangu kuingia madarakani kwa Rais Magufuli alieleza masikitiko yake kwa nchi kushindwa kunufaika na madini yaliyopo nchini.

Katika kipindi hicho yalifanyika marekebisho ya Sheria ya Madini sura ya 123 ambayo yamesaidia kuimarisha na kukuza sekta hiyo na kuiwezesha kuongeza mchango wake katika pato la Taifa.

Aidha, mafanikio mengine yaliyoletwa na wizara hiyo ni kutolewa kwa leseni 221 za uchenjuaji madini, leseni 4 za uyeyushaji madini (smelting) na leseni 4 za usafishaji madini (refining), pia, kutenga hekta 38,567 kwa ajili ya uchimbaji mdogo na kuwapatia mafunzo wachimbaji wadogo 10,338.



**SELEMANI JAFO**

Waziri mwingine kijana ni Waziri wa TAMISEMI, Selemani Jafo, ambaye ni Mbunge wa Kisarawe, aliingia kwenye baraza hilo mwaka 2015 akiwa ni naibu, na kwa kipindi chote amefanya kazi nzuri ambayo mara kwa mara Rais ameisifia.

Kwa kipindi cha miaka minne wizara hiyo imesimamia ujenzi na ukarabati wa hospitali za halmashauri 98, vituo vya afya 433 na zahanati 368, huku upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ukiwa wa uhakika kwa asilimia 92.

Aidha, kwa kipindi hicho serikali ilitumia jumla ya Sh. trilioni 1.01 kugharamia mpango wa elimu bure pamoja na miundombinu ya shule za msingi na sekondari.

Pia, vyumba vya madarasa 19,808 vimekamilika na nyumba 1,313 zipo katika hatua za ukamilishaji, maabara za masomo ya sayansi 227 zimejengwa na shule za sekondari 1,258 zimapatiwa vifaa vya maabara.

Matundu ya vyoo 7,922 yamejengwa na kukamilika na 571 yanaendelea kukamilishwa na madawati 5,070,896 yalitengenezwa na shule kongwe za sekondari 73 zilikarabatiwa.

Aidha, jumla ya Sh. bilioni 93.3 zilielekezwa kwenye vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

TAMISEMI kwa miaka minne imesimamia ukarabati na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 74,940.06 kati yake kilomita 485 zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Pia, jumla ya madaraja 232 na makalavati 7,168 yamejengwa na kukamilika.

**UMMY MWALIMU**



Mwingine ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum, umahiri wake ulionekana zaidi wakati wa janga la corona kwa kusimama imara na kuhakikisha nchi inavuka salama, kiasi cha Rais kumsifia hadharani mara kwa mara.

Mafanikio yake yamejikita katika kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za chanjo ili kuwakinga watoto chini ya miaka mitano dhidi ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

Kuimarisha hali ya lishe na usafi wa mazingira ili kuwezesha wananchi kujikinga na magonjwa, kuboresha huduma za afya ya uzazi, Mama na Mtoto, na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wa chini ya miaka mitano.

Mingine ni kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya na kuboresha miundombinu na utoaji huduma katika hospitali zote za rufani za mikoa, pamoja na kuimarisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda nchini.

**INNOCENT BASHUNGWA**

Waziri mwingine kijana ni Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, ambaye amimudu sekta hiyo na kuleta mafanikio makubwa ikiwamo katika kipindi cha kupambana na janga la corona kuwa na viwanda vinavyotengeneza vifaa vya kujikinga.

Bashungwa ambaye ni Mbunge wa Karagwe, anachojivunia ni sekta hiyo kuchangia pato la taifa kwa asilimia 8.5 kutoka 8.05 mwaka 2018.

Jingine ni kasi ya ukuaji wa thamani ya uzalishaji bidha viwandani kwa mwala 2019 ilikuwa Sh. trilioni 10.2 ikilinganishwa na Sh. trilioni 9.6 mwaka 2018 huku kasi ya ukuaji ikiwa ni asilimia 5.8.

**ANTHONY MVUNDE**

Mwingine ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mvunde, ambaye amedumu katika nafasi hiyo toka kwaka 2015 na amefanikiwa kusimamia vyema katika programu za kurasimisha vijana.

Mavunde ambaye ni Mbunge wa Dodoma Mjini, alishughulikia changamoto za wafanyakazi kwenye sekta binafsi hasa viwanda ambako raia wa kigeni walikuwa wakiwanyanyasa wazawa.

**JUMAA AWESO**

Naibu Waziri aliyeingia na kuonyesha uwezo wake ni Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ambaye ni Mbunge wa Pangani alifanyakazi kuhakikisha upatikanaji wa maji na ufanisi katika miradi ya maji ambayo mingi imekuwa kichefuchefu kwa kuwa inatumia mabilioni ya fedha na kushindwa kutoa maji.

Amekuwa msaada mkubwa kwa waziri wake, Profesa Makame Mbarawa katika kusukuma utekelezaji wa miradi ya maji.

Kwa sasa hali ya upatikanaji wa maji vijijini ni asilimia 85 na miradi inayotekelezwa vijijini ili kuongeza upatikanaji wa maji ni 558, na kati yake 268 ina uwezo wa kuhudumia wananchi 1,539,509 kupitia vituo 7,540 katika vijiji 880 na itakamilika mwaka huu.

Aidha, wizara hiyo imekuja na mfumo wa 'force account' utakaopunguza gharama za utekelezaji wa miradi ya maji.

## HABARI KITAIFA

# Serikali yajizatiti kukuza utalii wa ndani

**Na Mwandishi Wetu**

MPANGO mpya wa kukuza utalii wa ndani unatarajiwa kuzinduliwa Julai 1, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya uzinduzi wa mkakati huo sambamba na viongozi wengine waandamizi kutoka serikali na wadau wa utalii nchini.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mpango huo, Mkumbwa Ally, mpango huo unaojulikana kama Domestic Tourism Promotion Initiative (DTPI) unalenga kutangaza utalii wa ndani kwa Watanzania pamoja na raia wa kigeni kuhusu vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

"Ni mpango unaohusisha juhudi mahsusi katika kusaidiana na serikali kukuza utalii wa ndani na kupunguza athari za janga la corona kwenye sekta hii muhimu," alisema Mkumbwa.

Mkakati huo wenye kauli mbiu 'Utalii Mpya, Fursa Mpya' unaratibiwa kwa pamoja kati ya Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino Tanzania (SAUT) na kampuni ya Real PR Solutions ya jijini Dar es Salaam.

Alisema hafla hiyo fupi itahusisha pia ushiriki wa viongozi waandamizi wa serikali na wadau mbalimbali wa sekta ya utalii wakiwamo Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (TATO), Chama cha Watoa Huduma za Utalii wa Ndani (TLTO) na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Wengine ni Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania (TFS), Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Chama cha Wamiliki wa Hoteli na wadau wengine.

"Zaidi pia tumewaalika Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Waziri wa Afya kutokana na michango yao katika ustawi wa sekta ya utalii hapa nchini," alisema.

Alitaja baadhi ya mambo muhimu kwenye kampeni hiyo ambayo yatatekelezwa kwa awamu kuwa ni mafunzo kwa vijana kote nchini, ili waweze kunufaika na mnyororo wa thamani katika sekta ya utalii ikiwamo kuongoza watalii, mafunzo ya huduma kwa wateja katika hoteli na migahawa, vyombo vya usafiri na ujuzi wa kufungua kampuni za utalii.

"Tunatarajia mafunzo haya yatawanuisha vijana zaidi ya 100,000 hususani wale wasio na ajira ili waweze kutambua fursa zilizopo kwenye sekta ya utalii na wazitumie vizuri," alisema Mkumbwa, huku akiitaja mikoa itakayoanza kunufaika na mpango huo ni ya Kanda ya Ziwa ikiwamo Mwanza, Geita, Kagera, Simiyu, Mara na Shinyanga.

Alisema katika kuupamba mkakati huo, kutakuwa na uhusishwaji wa matukio mbalimbali ya kimichezo na burudani ili kuvutia walengwa zaidi wa mpango huo.

"Mkakakati huu unahusisha matukio mbalimbali yanayolenga kusaidia ukuaji wa sekta ya utalii nchini na kukuza uchumi wa ndani, lakini kuisaidia serikali na wafanyabiashara kuamsha tena biashara zilizokuwa zimezorota kufuatia janga hili la corona na hatimaye tukuze uchumi wa nchi," alisema Mkumbwa.

Alisema tahadhari zote za kiafya zitachukuliwa kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona katika matukio yote yaliyomo kwenye mpango huo. na sheria zilizowekwa.

# Moto ulivyozua taharuki kiwanda cha nguo Moro

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

TAHARUKI imetokea katika kiwanda cha kutengeneza nguo cha 21st Century cha Mjini Morogoro maarufu kama Polyester, baada ya kuibuka kwa moto kwenye jengo la idara ya ufumaji wa nyuzi.

Hili ni tukio karibu la tatu la moto katika kiwanda hicho, ambapo mwaka juzi jengo hilo pia lilishika moto, huku jengo la utengenezaji wa nguo (khanga) nalo likishika moto mwaka jana.

Nipashe ilishuhudia magari ya Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro na magari ya Polisi, yakiwa na askari waliowahi eneo la tukio kudhibiti moto huo usilete aathiri maeneo mengine ya uzalishaji kiwandani hapo, huku moshi ukiwa imetawala.

Meneja Utumishi wa kiwanda hicho, Nicodemus Mwaipungu, alipohojiwa, alisema hali hiyo ilisababishwa na shoti ya umeme kwenye eneo la idara ya weaving (ufumaji nyuzi) na kuunguza sehemu ya pamba iliyokuwapo na baada ya nusu saa wakaamua kuwaita watu wa Zimamoto na Uokoaji ili kuhakikisha kama wamefanikisha zoezi hilo.

"Sisi tuna idara ya fire hapa, tulipozima tukaona tuwaite Fire kwa sababu ni serikali, haukuwa moto mkubwa, ni shoti tu, na hakuna athari zozote kubwa zilizojitokeza, hata hii harufu mnayoisikia ni ile pamba kidogo iliyoungua na kusababisha moshi na kadri moshi unavyokwenda juu ndio harufu inatokea chini," alisema Mwaipungu.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Goodlucky Zelothe, alisema walipokea taarifa za tukio la moto majira ya saa moja usiku, na walipofika walikuta jitihada za wafanyakazi wa kiwanda kupambana na moto huo zinaendelea na ulikuwa bado ukiwaka kwenye paa zaidi na wakashirikiana kuudhibiti.

"Kwa haraka haraka inadaiwa umesababishwa na shoti ya umeme, lakini tutachunguza tujue zaidi, ila kifupi haujasababisha madhara makubwa, mitambo iko salama isipokuwa jengo hasa sehemu za paa, lakini taarifa zaidi tutatoa tukishafanya uchunguzi," alisema.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, alisema moto huo ulitokea kwenye mifumo ya umeme, na kwamba kiwanda walichukua hatua za haraka kwa kutumia miundombinu yake ya kukabiliana na moto.

"Kiwandani hali ni shwari, na uzalishaji unaendelea, kiwanda hiki ni muhimu kwa sababu kinatoa ajira kwa watu zaidi ya 2,000, na nimshukuru Rais kuendelea kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda... kuna wakati Morogoro ilikuwa ya viwanda, lakini viliporomoka na sasa tunarudisha viwanda," alisema na kuongeza:

"Lakini jitihada za kurudisha viwanda ni lazima ziendane sambamba na jitihada za kuvilinda viwanda na jitihada hizi ni pamoja na kuweka miundombinu mizuri ya kuzima moto."


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
President's Office – State House
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

**TENDER NO. TZ-TASAF-181607-GO-RFB TO SUPPLY THERMAL SCANNERS**

**Invitation for Tenders**

**Date: 26th June, 2020**

1. This Invitation for Tenders follows the General Procurement Notice for this Project which appeared in UN Development Business Issue no. WB-P475857-02/20 dated 4th February, 2020.

2. The Government of the united republic of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of the Productive Social Safety Net II. This project will be jointly financed by the Agency for International Development, Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria, International Fund for Agriculture Development, The government of NORWAY and OPEC. The Tanzania Social Action Fund the implementing agency for this Project intends to apply part of the proceeds toward payments for procurement of Thermal Scanners.

3. The The Tanzania Social Action Fund now invites sealed tenders from eligible Suppliers of Thermal Scanners.

4. Tendering will be conducted through the National Competitive tendering procedures specified in the Public Procurement Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 as amended in 2016, and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.

5. Interested eligible Tenders may inspect the Tendering Documents in the TASAF Website at: www.tasaf.go.tz or obtain further information through the address indicated below.

6. A complete set of Tendering Document(s) in English is available and can be downloaded from the TASAF Website at: www.tasaf.go.tz by interested Tenderers. Amendments and clarifications to the Tendering Documents if applicable will also be posted at the same Website.

7. All tenders must be accompanied by a Tender Securing Declaration in the format provided in the Tendering Documents.

8. All tenders must be addressed as indicated below and submitted via e-mail at or before 10:00 hours East African time on 10th July, 2020

   Electronic Tendering will not be permitted except e-mail submission as detailed in ITB BDS 21.2 in view of COVID-19. Late Tenders will be rejected.

   In view of COVID-19, the public opening will be conducted immediately after the deadline time for submission through live streamed and recorded and the video recorded will be posted for viewing through the TASAF's website: www.tasaf.go.tz. Online tender opening meeting details are indicated in ITB BDS 25.1.

9. Late Tenders, Portion of Tenders, Electronic Tenders, Tenders not received, Tenders not opened and not read out in public at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**Board of Trustee of PSSSF Building,**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**

215790302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars iandaliwe mapema kuelekea fainali za CHAN

**TIMU** ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ilifuzu kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani maarufu (CHAN), mashindano ambayo yanaandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Taifa Stars inayonolewa na Kocha Mkuu Mrundi, Etienne Ndayiragije, ilifuzu kushiriki fainali hizo kwa mara ya pili tangu zianzishwe baada ya kuwafunga Sudan hapo Oktoba mwaka jana.

Hii ni mara ya pili kwa Taifa Stars kukata tiketi ya kushiriki fainali hizo, kwa mara ya kwanza ilishiriki fainali hizo mwaka 2008 nchini Ivory Coast na Mbrazil Marcio Maximo ndio alikuwa Kocha Mkuu.

Hata hivyo, michuano hiyo kama ilivyokuwa katika mashindano mengine mbalimbali yaliyotarajiwa kufanyika, ilisimamishwa kutokana na janga la ugonjwa wa corona.

Aidha, CHAN ilipangwa kufanyika kuanzia Aprili 4 hadi 25, mwaka huu katika miji mitatu tofauti huko Cameroon.

Kwa sasa timu zote 16, zilizofuzu kushiriki fainali hizo, zinasubiri tarehe mpya ya mashindano ili kwenda kuwania taji hilo la pili kwa ukubwa hapa barani Afrika.

Michuano hiyo inashirikisha wachezaji wanaocheza ligi za ndani na kwa hapa nchini, kikosi chetu kinaundwa na nyota wengi wanaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo kwa sasa inaelekea ukingoni.

Nipashe linalikumbusha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuanza mikakati ya kuiandaa Taifa Stars ili ratiba ya mashindano hayo itakapotolewa wawe imara kwenda kupeperusha vema bendera ya nchi.

Tunaamini timu itakayoandaliwa vizuri, itakwenda kushindana na tuache mazoea ya kusubiri ratiba inapotoka ndio tunaanza kuandaa kikosi na matokeo yake badala ya kwenda kushindana, tunakwenda kuwa wasindikizaji.

Ni vema TFF ikatekeleza mipango ya Ndayiragije ya kukijenga kikosi cha Stars kwa kutafuta mechi mbalimbali za marafiki kabla ya kuanza kwa fainali hizo.

Hii inatokana na viwango vya wachezaji wa Stars hasa kwa kuzingatia ubora wa Ligi Kuu Tanzania Bara na ligi wanazotoka wachezaji wa timu wapinzani watakazokutana nazo.

Mara nyingi maandalizi ya zimamoto yamekuwa yakifanya na Stars au timu yoyote kwenda katika mashindano kukamilisha ratiba badala ya kwenda kuchukua kikombe.


Mbali na kupata taji, mashindano hayo ni sehemu nyingine ya kutangaza vipaji vya wachezaji wa Kitanzania ambao wengi bado wana ndoto za kwenda kucheza soka la kulipwa Ulaya, wanaweza kuonekana na mawakala wanaotafuta wachezaji.

Lazima tukumbuke wachezaji wengi wa Tanzania hawajapitia katika akademi za soka na hivyo kukosa baadhi ya misingi, kwa maana hiyo wanahitaji kupata muda mrefu zaidi wa maandalizi tofauti na nyota watakaokutana nao kutoka mataifa yaliyopiga hatua kama Misri, Algeria au Afrika Kusini.

Pia Stars imetinga katika hatua ya makundi katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo la Kombe la Dunia, michuano ambayo mechi zake huwa na ushindani zaidi kwa sababu kila nchi inajua umuhimu wa kupeperusha bendera yake kwenye michuano hiyo.

Ili Stars iende katika mashindano yote ikiwa imara, wadau wote wanatakiwa kushiriki katika maandalizi kuanzia sasa kwa ushirikiano na TFF na kuacha tabia ya kusubiri kulaumu pale wawakilishi wetu hao watakapofanya vibaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Azam ipo ipo tu, haina presha

**BAADA** ya muda mrefu kupita ikishika nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, hatimaye Azam imeteremka hadi kwenye nafasi ya tatu.

Kwa sasa nafasi ya pili inashikiliwa na Yanga iliyofikisha pointi 60, huku Azam ikiwa imesalia pointi zake 59.

Hii ni baada ya Yanga kuichapa Ndanda mabao 3-2 na Azam kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Biashara United mjini Musoma.

Ingawa bado Ligi Kuu inaendelea na Azam inaweza kumaliza ikiwa kwenye nafasi ya pili, lakini kwa sasa iko kwenye wakati mgumu kwani imekuwa haipati matokeo mazuri.

Kwa muda mrefu, Azam ilikuwa inashika nafasi ya pili tena kwa pointi nyingi, lakini Yanga ambayo msimu huu haikuonekana ipo vizuri, tena ikiwa na sare nyingi sana, lakini imejivuta hadi kufika kwenye nafasi ya pili.

Hata kama Azam itarejea tena kwenye nafasi ya pili, lakini kwa jinsi ilivyo itapata shida sana. Ukizitazama timu hizi mbili, Yanga na Azam ni vitu viwili tofauti.

Azam inaonekana iko vizuri zaidi, ikiwa na wachezaji wenye vipaji na uwezo wa hali ya juu, pia kitimu inaonekana iko vizuri zaidi na ni timu yenye uwezo hata ya kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara.

Kwa upande wa Yanga msimu huu, bado inaonekana inajikongoja tu. Siyo ile Yanga iliyozoeleka.

Huwezi kulinganisha uwezo wa wachezaji mmoja mmoja wa Yanga na wa Azam.

Bado Yanga ina wachezaji wa kawaida sana na ni wachache ambao wana uwezo mkubwa na kuweza kuingia kwenye kikosi cha kwanza cha Azam.

Tatizo ni nini hata Azam imeshindwa kufukuzana hata na Simba huko juu kileleni kwenye mbio za kutwaa ubingwa, achilia mbali kukutwa na kupitwa na Yanga?

Ni kwamba Azam pamoja na kwamba ni timu yenye wachezaji wenye uwezo mkubwa, lakini inakosa watu wa kuwasukuma.

Inakosa watu wa kuwapigia kelele pale wanapofanya vibaya. Inakosa watu wa kuwakumbusha majukumu yao na kuwafanya wapambane kwa ajili yao. Si wengine ni mashabiki.

Kinachozitofautisha timu za Simba, Yanga na ile ya Azam ni mashabiki.

Mfano Yanga ambao kwa misimu miwili sasa haijakaa vizuri, lakini inapambana kwa sababu nyuma yake kuna mashabiki wanaoisukuma.

Hata kama ina wachezaji wa kawaida, lakini kuichezea Yanga inabidi upambane kufa na kupona kusaka ushindi ili kuwafanya wawe wa furaha.

Na hata wanapoukosa, wachezaji wa timu hiyo wanaona joto la jiwe. Mashabiki wanawashambulia kwa maneno mengi, hivyo wanapokwenda kwenye mechi inayofuata wanakuwa wamejiandaa kisawasawa.

Ikumbukwe ni majuzi tu, mashabiki wa Yanga walikuwa wakimpigia kelele Gnamien Yikpe na hata David Molinga kuwa hawawaelewi.

Lakini mechi iliyofuata dhidi ya Namungo, Molinga alirekebisha makosa yake, akajituma na kufunga magoli mawili.

Hata Simba, inaweza kushinda hata mechi sita mfululizo, lakini ya saba ikitoa sare, tayari mashabiki wanakuja juu na kuwatupia lawama wachezaji wao kuwa wanaishi vizuri, wanapata mishahara mizuri, lakini hawajitumi. Mechi inayofuata wachezaji wanafanya kila njia ili kupata ushindi.

Hili halipo kwa Azam. Hata wao waishi na kupata stahiki zao zote, lakini hawapati ushindi mara kwa mara kwa sababu, wakishinda sawa, wakifungwa poa na hata wakitoka sare hakuna tatizo.

Hakuna mtu wa kuwapigia kelele. Hakuna mtu wa kuwauliza. Wachezaji wanapanda basi na kuondoka kama vile hakuna kilichotokea. Hata mechi inayofuata inakuwa hivyo hivyo.

# Wanawake walia rushwa ya ngono kupata uongozi

**Na Elizabeth Zaya**

WANAWAKE wa kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Ukonga jijini Dar es Salaam, wamesema kuwa tatizo la rushwa ya ngono limeendelea kuwa kikwazo kwa wanawake wengi kushindwa kupata nafasi za uongozi katika nyanja mbalimbali.

Walitoa kauli hiyo katika semina maalum jijini Dar es Salaam, iliyolenga kuwapatia elimu wanawake hao namna ya kupambana na vitendo hivyo vya ukatili iliyodhaminiwa na Taasisi ya Women Fund.

Lucy Makula, Msaidizi wa kisheria Kipunguni na Mjumbe wa Sauti ya Jamii, alisema tatizo hilo la rushwa limekuwa likiwakatisha tamaa wanawake wengi wanapoomba ajira katika taasisi mbalimbali na pia katika nafasi ya uongozi kwenye siasa.

"Sijui kama jambo hili litaisha, wanawake tumekuwa tukipambana sana lakini tunarudishwa nyuma na watu wasiotutakia mema, kuna shuhuda nyingi sana za wanawake au wasichana kuomba rushwa ya ngono wanapokwenda kuomba nafasi za ajira na wengi wanakosa kwa sababu ya kukataa kutoa rushwa hiyo," alisema Makula.

"Kwenye siasa ndiyo usiseme, huko tena ndiyo hatari. Angalau msichana mwenye umri mdogo anaweza kufikiriwa kupewa nafasi kwa lengo la kwamba aingie ili wamuombe rushwa ya ngono au wanapendekeza jina lake halafu wanajitokeza watu kila mmoja kwa wakati wake wanakuwa wanamshawishi atoe rushwa ili wampitishe."

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii Kata za Msongola na Kivule, Msekwa Joliga, alisema wamekuwa wakipokea kesi nyingi zinazohusiana na rushwa ya ngono.

"Ni kweli tunapata kesi nyingi za ambazo wanawake na wasichana wamekuwa wakija kulalamika kwamba wanaombwa rushwa ya ngono aidha na viongozi katika nyanja mbalimbali wanapokwenda kutafuta huduma au nafasi za uongozi na tumekuwa tukipambana kuyashughulikia na kuwashauri pia," alisema Joliga.

Sheikh Abdi Mahanyu kutoka eneo hilo, alisema imefika wakati ambao wanawake nao wanahitaji kubadilika kwa kuacha kufumbia macho au kuwaficha watu wanaofanya vitendo hivyo vya unyanyasaji badala yake wahakikishe wanatoa taarifa katika vyombo vya dola ili wahusika wachukuliwe hatua.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Josephat Kandege (katikati), akiongea jambo na Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Mashariki, Baraka Ladislaus (kushoto), baada ya benki hiyo kutoa msaada wa mabati 160 kwa Shule ya Sekondari Magindu iliyopata mabati 106 na Shule ya Sekondari Msagani mabati 54 yote yakiwa na thamani ya shilingi milioni 5, katika hafla iliyofanyika Shule ya Sekondari ya Zogowale Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani. Kulia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Assumphta Mshama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakurugenzi wazembe bodi za mazao sasa kutumbuliwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ametangaza kuwa atawaondoa kwenye nafasi zao wakurugenzi wa bodi za mazao ya kipaumbele ambao watashindwa kukamilisha usajili wa wakulima wa mazao husika baada ya Juni 30, mwaka huu.

Waziri Hasunga alitoa tangazo hilo mwishoni mwa wiki katika Kata ya Lupatingatinga Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, alipokuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa masoko ya tumbaku nchini kwa ajili ya msimu wa kilimo wa 2019/2020.

Alisema alishatoa maagizo kwa wakurugenzi wa bodi hizo kuwasajili wakulima kwa kuzingatia aina ya mazao wanayozalisha, ukubwa wa maeneo wanayolima pamoja na matatizo wanayokabiliana nayo kwenye kilimo cha mazao husika ili kuirahisishia serikali namna ya kuwahudumia.

"Baada ya Juni 30 nitachukuwa hatua dhidi ya wakurugenzi wote ambao watashindwa kukamilisha usajili wa wanakulima, sasa nimefuatilia nimeona hata wewe Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku (TTB), hujakamilisha hilo zoezi, sasa sijui nitaanza na wewe?" Alihoji Hasunga.

Hata hivyo, aliwataka viongozi wa vyama vikuu vya wakulima wa tumbaku kuhakikisha wanashirikiana na Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku na viongozi wengine wa serikali kwenye maeneo husika kutatua matatizo yanayolikabili zao hilo.

Katika hatua nyingine, Waziri Hasunga aliwataka maofisa kilimo wa wilaya, kata na vijiji kuacha kukaa ofisini, badala yake wawatembelee wakulima mashambani kwa ajili ya kuwashauri kuhusu mbinu za kilimo bora cha mazao wanayozalisha ili kuongeza tija.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kuacha kuwapangia majukumu mengine ikiwamo ukusanyaji wa mapato na kwamba endapo atamkuta ofisa kilimo yeyote akiwa amekaa ofisini, atamfuta kwenye orodha ya maofisa hao.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TTB, Stanley Mnonzya, alisema moja kati ya matatizo yanayowakabili wakulima wa tumbaku ni kampuni zinazonunua zao hilo kuchelewesha malipo ya wakulima hali ambayo inasababisha wakulima kushindwa kufikia malengo.

Alisema ili kutatua tatizo hilo, Bodi ya Tumbaku inakusudia kuanza kuzichukulia hatua za kisheria kampuni za ununuzi wa zao hilo ambazo zitashindwa kuwalipa wakulima malipo yao ndani ya siku 14 kuanzia siku ambayo zinachukua mazao yao.

Alisema zao la tumbaku linapita katika kipindi cha mpito kuanzia msimu wa kilimo wa mwaka 2014/2015 kwa kuwa soko lake limekuwa likisuasua kutokana na baadhi ya wanunuzi kujiondoa kwenye ununuzi kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo kodi nyingi.

Mwishoni mwa wiki Waziri Hasunga alizindua soko la tumbaku katika Chama cha Msingi cha Lupatingatinga wilayani Chunya, soko ambalo liliwakilisha uzinduzi wa masoko mengine katika mikoa 12 nchini inayozalisha zao hilo.

# Wanahisa CRDB kupata gawio la bilioni 44.4/-

**Na Mwandishi Wetu**

WANAHISA wa Benki ya CRDB wameidhinisha gawio la shilingi 17 kwa hisa lililopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi ya benki hiyo katika Mkutano Mkuu wa 25 wa Wanahisa uliofanyika Jumamosi kidijitali, na jumla ya gawio la Sh bilioni 44.4 zilitolewa.

Wakichangia maoni ya kupitisha pendekezo hilo la ongezeko la gawio kwa asilimia 112.5, wanahisa wamepongeza uongozi na wafanyakazi wa benki hiyo kwa matokeo mazuri yenye tija kwa wanahisa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay, alisema ukuaji wa gawio kwa wanahisa kutoka shilingi 8 kwa hisa mwaka jana hadi shilingi 17 kwa hisa, umechangiwa na matokeo mazuri ya kifedha ambapo ilipata ongezeko la faida kwa asilimia 87 kufikia shilingi bilioni 120.1 kulinganisha na shilingi bilioni 64 mwaka 2018.

"Matokeo haya yamesababisha bodi kupendekeza gawio la shilingi 17 kwa hisa ambalo ni historia kwa benki yetu," alisema Dk. Laay huku akiwapongeza wa wanahisa kwa kushiriki kwa wingi zaidi katika mkutano huo uliofanyika kidijitali.

Dk. Laay alisema mwaka 2019 ulikuwa wa mafanikio kwa Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu za Benki ya CRDB Burundi na kampuni tanzu ya Bima. "Katika kampuni tanzu ya Burundi tumefanikiwa kupata ongezeko la faida la asilimia 146 wakati kwa upande wa kampuni yetu tanzu ya Bima tumefanikiwa kupata ongezeko la faida kwa asilimia 17," alisema huku akisema kuwa mkakati wa benki hiyo kupanua wigo wake katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati unaoendelea, huku benki hiyo ikiangazia kupanua wigo katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Akiwasilisha ripoti yake, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema katika mwaka wa fedha wa 2019 Benki ya CRDB imeshuhudia ukuaji mkubwa katika biashara yake ambapo amana za wateja ziliongezeka kwa asilimia 8 kufikia shilingi trilioni 3.4 kulinganisha na shilingi trilioni 3.1 mwaka 2018, rasilimali ziliongezeka kwa asilimia 11 kufikia shilingi trilioni 6.6 kulinganisha na na shilingi trilioni 5.2 mwaka 2018.

"Tulifanikiwa pia kupanua wigo wa wateja wetu kwa zaidi ya asilimia 50, sasa hivi tuna zaidi ya wateja milioni 3 ukilinganisha na wateja milioni 2 tuliokuwa nao hapo awali," alisema Nsekela. Nsekela alisema mafanikio hayo yanatokana na jitihada kubwa zilizofanya na benki hiyo katika kuingiza bidhaa na huduma bunifu na zinaoendana na mahitaji ya wateja katika soko.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo, alisema benki hiyo imeendelea kuimarika zaidi hususani katika upande wa utoaji mikopo, huku akibainisha kuwa imefanikiwa kupunguza mikopo chechefu kwa asilimia 35 huku uwiano wa mikopo chechefu ukipungua kutoka asilimia 8.3 hadi kufikia asilimia 5.5.

Katika mkutano huo, wanahisa wa waliwachagua Prof. Neema Mori na Miranda Mpogolo kuwa wajumbe huru wa Bodi ya Wakurugenzi, huku Dk. Edwin Mhede akitambulishwa kama mjumbe mpya wa Bodi akiwakilisha Mfuko wa Uwekezaji wa DANIDA.

# Balozi Seif: Wanachama CCM pokeeni fedha za wagombea

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, amewataka wanachama wa CCM mkoani Shinyanga, kutosita kupokea fedha watakazohongwa na wagombea kwenye uchaguzi mkuu.

Badala yake wasiwapigie kura na kuwaripoti kwenye Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na wanachama wa chama hicho kutoka katika Halmashauri za Msalala, Kahama Mjini na Ushetu, baada ya kupokea taarifa kuhusiana na maandalizi ya uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba mwaka huu.

Alisema kuna wagombea ambao wanapita kwa wanachama hasa kwenye matawi, kata, wilaya hadi mkoa na kuwapatia fedha wanachama kiasi cha shilingi 5,000 hadi 20,000.

Balozi Seif alisema CCM haitapitisha jina la mgombea yeyote atakayebainika kutoa fedha ili kupata nafasi ya kuchaguliwa, hata kama atakuwa amepitishwa na mkutano mkuu ndani ya chama.

"Wapambe wa wagombea wameanza kupitapita katika matawi, kata na wilaya na kugawa fedha kiasi cha Sh. 5,000 hadi 20,000, zipokeeni lakini msiwachague kwa sababu CCM inautaratibu wake wa kuwapata viongozi na ikiwezekana waripotini TAKUKURU," alisema.

Alisema: "Vyombo vyetu vya dola vimejipanga kikamilifu kudhibiti vitendo vya rushwa ambavyo husababisha wagombea wenye sifa kutochaguliwa na wasiokuwa na sifa kuchaguliwa. Vitendo hivyo vimekuwa vikikikosesha chama ushindi kwenye chaguzi zake."

Kaimu Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Gaspar Kileo, aliwataka makatibu wa matawi, kata na wilaya kuwachukulia hatua kali watia nia ambao watakaobainika kuanza kampeni mapema kabla ya muda.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Godfrey Ndalahwa, akizungumza na wanahisa wakati wa Mkutano Mkuu wa 18 wa Wanahisa wa benki hiyo, ulifanyika kwa njia ya mtandao jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Mwanasheria wa Kampuni, Alex Mgongolwa, Mkurugenzi wa Sheria wa DCB na Katibu wa Kampuni, Regina Mduma, Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya DCB, Prof. Lucian Msambichaka na Mjumbe wa Bodi ya benki hiyo, Zawadia Nanyaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Wawekezaji wahakikishiwa mazingira rafiki

**Na Mwandishi Wetu, MBEYA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji ), Angela Kairuki, amewahakikishia wawekezaji wenye viwanda Nyanda ya Juu Kusini kuwa serikali inashughulikia changamoto mbalimbali.

Miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa ni kwa nishati na miundombinu mingine ya uhakika lengo likiwa kuongeza uzalishaji na kuchochea ukuaji wa sekta ya viwanda nchini.

Sambamba na hilo, Waziri Kairiki amesema serikali ambayo imeazimia kujenga uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025, ilishachukua hatua mbalimbali muhimu kuweka mazingira mazuri yatakayovutia uwekezaji.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kuhitimisha ziara yake katika ushoroba wa kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) kwa kutembelea viwanda vya Tukuyu Srings Water, Raphael Group Limited, Stawisha (Dutch Potato Project), Tanzania Breweries Limited ( TBL) na Marmo Granito Mine ( T) Ltd, Kairuki, alisema serikali inatambua umuhimu wa uwekezaji katika kuinua uchumi.

"Ninawapongeza kwa uwekezaji huu wenye uhakiki na kwa upande wa serikali tutaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini. Kwa upande wa serikali imeshachukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa mazingira ya kuwekeza yanaendelea kuwa rafiki," alisema.

Aliipongeza SAGCOT kwa kushirikiana na wadau wake kwa kazi nzuri wanayofanya katika katika ushoroba huo kuhakikisha wanaboresha na kuwajengea uwezo wakulima wadogo na kati kwa kuwafundisha mbinu za kilimo chenye tija ambacho kimekuwa na matokeo chanya katika kujikwamua kiuchumi na kuchochea uwekezaji eneo hilo.

Waziri alisema kuwapo kwa Ofisi ya Kanda ya Kituo cha Uwekezaji (TIC) katika mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa hatua thabiti serikali imekuwa ikizichukua kuhakikisha kuwa wawekezaji wanapata huduma kwa karibu zaidi.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Raphael Group Limited, kinachojihusisha kuongeza thamani ya mazao ya nafaka, Raphael Ndelwa, aliipongeza SAGCOT kwa kuwafungulia njia ya kibiashara kwa kuwaunganisha na taasisi za kilimo pamoja na kukidhi mahitaji ya kiwanda.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Stawisha linalojihusisha na kilimo cha viazi mviringo, Theresia Mcha, alisema shirika lao linafanya kazi kwa ukaribu sana na wakulima wa viazi mviringo na kuhimiza kilimo bora cha viazi na kuongeza tija.

# Serikali sasa yajizatiti kukuza utalii wa ndani

**Na Mwandishi Wetu**

MPANGO mpya wa kukuza utalii wa ndani unatarajiwa kuzinduliwa Julai 1, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya uzinduzi wa mkakati huo sambamba na viongozi wengine waandamizi kutoka serikali na wadau wa utalii nchini.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mpango huo, Mkumbwa Ally, mpango huo unaojulikana kama Domestic Tourism Promotion Initiative (DTPI) unalenga kutangaza utalii wa ndani kwa Watanzania pamoja na raia wa kigeni kuhusu vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

"Ni mpango unaohusisha juhudi mahsusi katika kusaidiana na serikali kukuza utalii wa ndani na kupunguza athari za janga la corona kwenye sekta hii muhimu," alisema Mkumbwa.

Mkakati huo wenye kauli mbiu 'Utalii Mpya, Fursa Mpya' unaratibiwa kwa pamoja kati ya Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino Tanzania (SAUT) na kampuni ya Real PR Solutions ya jijini Dar es Salaam.

Alisema hafla hiyo fupi itahusisha pia ushiriki wa viongozi waandamizi wa serikali na wadau mbalimbali wa sekta ya utalii wakiwamo Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (TATO), Chama cha Watoa Huduma za Utalii wa Ndani (TLTO) na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Wengine ni Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania (TFS), Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Chama cha Wamiliki wa Hoteli na wadau wengine. "Zaidi pia tumewaalika Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Waziri wa Afya kutokana na michango yao katika ustawi wa sekta ya utalii hapa nchini," alisema.

Alitaja baadhi ya mambo muhimu kwenye kampeni hiyo ambayo yatatekelezwa kwa awamu kuwa ni mafunzo kwa vijana kote nchini, ili waweze kunufaika na mnyororo wa thamani katika sekta ya utalii ikiwamo kuongoza watalii, mafunzo ya huduma kwa wateja katika hoteli na migahawa, vyombo vya usafiri na ujuzi wa kufungua kampuni za utalii.

"Tunatarajia mafunzo haya yatawanuisha vijana zaidi ya 100,000 hususani wale wasio na ajira ili waweze kutambua fursa zilizopo kwenye sekta ya utalii na wazitumie vizuri," alisema Mkumbwa, huku akiitaja mikoa itakayoanza kunufaika na mpango huo ni ya Kanda ya Ziwa ikiwamo Mwanza, Geita, Kagera, Simiyu, Mara na Shinyanga.

HABARI KITAIFA

# Wazazi watakiwa kufuatilia taaluma ya watoto kidigitali

Na Enock Charles

WAZAZI wameshauriwa kuendelea kutumia mfumo wa kidigitali kufuatilia maendeleo ya kitaaluma kwa watoto wao wanaosoma shule za msingi na sekondari nchini, ili kusimamia vyema elimu kwa watoto hao.

Akizungumza na vyombo vya habari, mwishoni mwa wiki iliyopita Mkurugenzi wa ShuleSoft inayohusika na kutoa elimu kwa njia ya mtandao, Ephraim Swilla, alisema licha ya tatizo la corona kupungua na wanafunzi kuruhusiwa kurejea shule kuendelea na masomo katika mfumo rasmi, lakini kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia ni muhimu kwa wanafunzi, walimu na wadau kuendelea kutumia mfumo wa elimu kwa njia ya mtandao.

"Kipindi hiki ambacho shule zinakwenda kufunguliwa mfumo wa ShuleSoft unaendelea kusaidia shule katika mambo kadha wa kadha ikiwamo kusimamia taaluma ya shule kwa kuandaa ripoti za kisasa na zenye ubora," alisema Swilla.

Mkurugenzi huyo alisema mfumo huo kwa sasa unafanya kazi na shule zaidi ya 400 nchi nzima ambazo ni shule za msingi na sekondari, huku malengo yao ikiwa ni kufikia shule nyingi zaidi na hata baadhi ya vyuo nchini na kwamba walimu walionao ni taaluma mbalimbali na uwezo mzuri wa kufundisha masomo yote kwa mujibu wa mitaala iliyopo.

Alisema pia kuwa mfumo huo umeboreshwa zaidi na kuwezesha usimamizi wa taaluma za wanafunzi kwa kuandaa ripoti zenye ubora, kurahisisha makusanyo ya ada kwa njia ya mtandao, kurahisisha uandaaji wa mishahara kwa kuchakata taarifa za watumishi wote, kuandaa ripoti za kifedha kwa urahisi na ufanisi na kuboresha mawasiliano na wazazi, ambapo wazazi hupata taarifa za shule kwa njia ya SMS, barua pepe, telegram na kuingia kwenye akaunti zao katika mfumo wa ShuleSoft.

# Sababu ndege za Tanzania kupeleka mazao ya bustani nje

Na Ashton Balaigwa, MBEYA

SERIKALI imekusudia kuuza mazao ya bustani yakiwamo ya mboga, viungo na matunda katika nchi za Asia na Ulaya kwa kuyasafirisha kwa kutumia ndege zake mpya ilizozinunua hivi karibuni.

Hatua hiyo inatokana na mazao hayo kuhitajika katika masoko ya nchi hizo, huku ikitarajia kujenga soko kubwa jijini Dar es Salaam ili yasafirishwa nchini inunuliwe na mataifa mengine.

Lengo la maamuzi hayo ya serikali ni kupambana na ujanjaujanja unaofanyika katika soko nchini Kenya, ambapo baadhi ya matunda na mboga yanayozalishwa nchini yanapelekwa nchini humo kuuzwa nje ya nchi na kuonekana yamezalishwa humo. Mazao hayo ni pamoja na parachichi na chai inayouzwa katika masoko ya Mombasa na Nairobi.

Kauli hiyo ya serikali ilitolewa na Waziri wa Kilimo, Japhet Husunga, wakati akizindua maonyesho ya kilimo biashara yanayofanyika katika mashamba darasa ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI-Uyole) iliyopo mkoani Mbeya yenye lengo la kuwabadilisha wakulima kutoka katika kilimo cha kujikimu ili kulima kilimo biashara pamoja na kuzungumza na watafiti wa taasisi hiyo.

"Mwaka jana sisi wenye eneo kubwa katika sekta ya bustani tumepata dola milioni 779 wakati Kenya kwenye sekta hiyo wamepata zaidi ya dola bilioni 6 wanatumia ujanja wa maparachichi yetu kuchukuliwa na kupelekwa Kenya, wanaenda kuuza nje kwa kuweka lebo ya Kenya... sasa tunataka kukomesha ujanja huo tunaanza kupeleka wenyewe kwenye masoko hayo ya Ulaya na Asia kwa kutumia ndege zetu," alisema Hasunga.

Alisema mazao ya mboga na matunda yatasaidia kuongezea Taifa fedha za kigeni zitakazotokana na kilimo hicho baada ya kupungua fedha hizo zilizokuwa zikiingia kutokana na utalii kufuatia ugonjwa wa COVID-19 ulioikumba dunia.

Hasunga alisema kuwa mojawapo ya mikakati mingine ya kuingiza serikali fedha za kigeni ni kupitia kilimo na kujenga soko kubwa la chai katika Jiji la Dar es Salaam ili chai inayozalishwa nchini iuzwe hapa.

Alisema ili kufikia mikakati hiyo, serikali imeanza mpango wa kuongezea TARI fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa kuzalisha mbegu bora za kisasa na zenye tija na kuongeza uzalishaji wa mazao hayo yatakayoiingizia Taifa fedha za kigeni ili yaweze kuzalishwa kwa wingi nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema kuwa wapo tayari kuzalisha mbegu mama za mazao hayo ya bustani, mboga na matunda kwa kuvitumia vituo 17 vya taasisi hiyo ya kilimo Tanzania kwa lengo la kusaidia serikali kuingiza fedha za kigeni.

Alisema TARI imekuwa ikizalisha mbegu teknolojia ya kisasa ya mazao ya mafuta ikiwamo zao la michikichi, alizeti na karanga kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mafuta nchini na hivi karibuni imepewa jukumu jipya la kuzalisha mbegu za zao la mkonge kwa kutumia vituo vyake vya utafiti na zinafanya vizuri katika uzalishaji.

Akizungumzia maonyesho hayo ya kilimo biashara, Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema yamelenga kuzifikisha teknolojia mpya zilizofanyiwa utafiti moja kwa moja kwa wakulima ili kuachana na kilimo cha kujikimu na kulima kibiashara.

Alisema hatua hiyo inatokana na nchi hivi sasa kuelekea katika uchumi wa viwanda hivyo malighafi kubwa itakayohitajika inatokana na mazao yanayotokana na kilimo, hivyo wameamua kuanza kuwaandaa wakulima kulima kwa kutumia mbegu zenye teknolojia ya kisasa ambazo zinaongeza tija kwa mkulima na kuwa na uhakika wa uzalishaji.

Mmoja wa wakulima ambaye amehudhuria maonyesho hayo, Shukuru Mwakibete, alisema kwa kupitia maonyesho hayo ameweza kujifunza mbinu mbalimbali katika kilimo cha viazi mviringo kwa kutumia mbegu za teknolojia za kisasa ambalo limekuwa ni la kibiashara hasa kwa wakazi wa Mkoa wa Mbeya.



Waziri wa Kilimo, Japhet Husunga (katikati), akisikiliza maelezo ya uzalishaji wa mbegu za mahindi kwa meneja wa shamba hilo, Onesmo Assenga (kushoto), alipotembelea Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI-Uyole) mkoani Mbeya. Kulia mwenye miwani ni Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo na kushoto kwa waziri ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Yohana Budeba. **PICHA: ASHTON BALAIGWA.**

# Kampuni za mafuta, gesi zatakiwa kuimarisha mifumo

Na Gwamaka Alipipi

MKUU wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, amezitaka kampuni zinazojishughulisha na biashara ya mafuta na gesi zilizomo wilayani humo, kuimarisha mifumo ya kulinda afya na usalama wa wafanyakazi ili kuepuka athari zinazoweza kutokea.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifungua kikao cha mashauriano baina ya wadau wa sekta ya mafuta na gesi pamoja na menejimenti ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kilichofanyika katika ofisi ya mkuu huyo Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

"Tunaweza kukwepa vyote, lakini hatuwezi kukwepa suala la usalama kwenye uendeshaji wa shughuli hizi, kwa bahati mbaya sana usalama huu hauwezi kusema wewe unajilinda kwa asilimia mia moja, kama wenzako waliokuzunguka hawana mifumo ya kujikinga kwa kiwango hicho, itakuwa ni kazi bure," alisema Msafiri.

Aidha, aliwataka wawakilishi wa kampuni za mafuta na gesi waliohudhuria kikao hicho kuwashauri viongozi wao wa juu katika kampuni wanazotoka kuwekeza katika masuala ya usalama na afya ili kuwalinda wafanyakazi pamoja na mali kwa ujumla.

Alisema uwekezaji katika usalama na afya una faida nyingi ikiwamo kuongeza morali miongoni mwa wafanyakazi, kuongeza ubora wa bidhaa na huduma na hivyo kuleta tija katika uzalishaji kwa manufaa ya wawekezaji na serikali kupitia mapato ya kodi.

Baadhi ya washiriki wa kikao hicho akiwamo, Leah John kutoka Kampuni ya Tipper na Moses Mgeni wa kampuni ya MOGAS, waliishukuru serikali kupitia OSHA kwa kuandaa kikao hicho.

Walieleza kuwa imekuwa ni fursa muhimu kwa pande zote mbili (OSHA na wadau) kujadiliana masuala ya msingi ambayo yatasaidia kuboresha mifumo ya usalama na afya katika sekta ya mafuta na gesi ambayo shughuli zake ni hatarishi zaidi kiusalama na afya.

# Maofisa wa ICT serikalini waonywa

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewaonya maofisa wanaohusika na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) serikalini kutochezea mifumo ili kujinufaisha binafsi kwani wamekuwa wakiisababishia serikali hasara.

Onyo hilo, lilitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, wakati akifunga mafunzo ya wiki moja kwa maofisa biashara wa mikoa ya Mwanza, Mtwara na Mbeya.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa ajili ya kuwaelimisha maofisa hao kazi za taasisi hiyo ili waweze kusajili wafanyabiashara kwenye mifumo yake wakiwa mikoani.

"Nyinyi maofisa TEHAMA ni watu ambao mnaisaidia sana serikali hasa kwenye kuongeza mapato, lakini msiendekeze vitendo vya rushwa maana kuna wakati mnachezea mifumo sasa vitendo hivi mara nyingi vinakuwa kikwazo na changamoto kubwa kwenye utoaji wa huduma," alisema Mhandisi Manyanya.

Manyanya alisema BRELA imefanya jambo jema kwa kuanza mchakato huo, lakini wanatakiwa kuharakisha kwenda kuelimisha maofisa wa mikoa mingine ili waweze kusajili wafanyabiashara wengi.

Alisema hatua hiyo imerahisisha kusogeza huduma za taasisi hiyo karibu na wananchi, hivyo kuwapunguzia gharama ambazo wangezitumia kusafiri umbali mrefu kuzifuata na kupoteza muda mwingi barabarani.

"BRELA mnatekeleza kwa vitendo, lakini hatuna muda wa kusubiri tunapaswa kwenda kwa haraka ili maofisa biashara na TEHAMA wa mikoa yote waweze kuongea sauti moja na mshirikiane na taasisi zingine kama WMA na TBS ili mtu akipata mafunzo haya ajue vitu vyote," alisema Manyanya.

# RC aeleza umuhimu elimu ya kodi kwa w'biashara

**Na Gwamaka Alipipi**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, amesema kampeni ya elimu kwa mlipakodi ambayo inaendeshwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), itawasaidia wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi kuacha vitendo hivyo ambavyo huikosesha serikali mapato.

Aliyasema hayo ofisini kwake wakati alipotembelewa na maofisa wa TRA wanaofanya kampeni hiyo mkoani hapa, ambayo imelenga kuwaelimisha wafanyabiashara kuhusu masuala ya kodi ikiwa ni pamoja na kuwakumbusha kulipa kodi kwa wakati.

Shigela alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakikwepa kulipa kodi pengine kwa kujua au kutokujua, jambo ambalo linahitaji elimu ya uelewa ili kila mwananchi afahamu wajibu wake kwenye eneo hilo kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Aidha, Shigela aliipongeza TRA kwa kuendesha zoezi hilo katika mikoa mbalimbali na kusema litaongeza ukusanyaji wa mapato.

"Zoezi hili litaleta mafanikio nchini baada ya wafanyabiashara kuelimishwa na kufahamu kuwa maendeleo ya nchi yanaletwa na ulipaji kodi kwa ajili ya kuboresha sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu, barabara, umeme na maji," alisema Shigela.

Shigela aliwataka wafanyabiashara kuhakikisha wanalipa kodi kwa hiari bila kusubiri kubugudhiwa na serikali, huku akieleza kuwa serikali itaendelea kupambana na wakwepa kodi wanaoingiza bidhaa za magendo nchini kwa kupitia bandari bubu zilizopo kandokando ya Bahari ya Hindi.

"Nchi yoyote haiwezi kupiga hatua ya maendeleo bila wananchi wake kuwa na utamaduni wa kulipa kodi kwa sababu kodi ndiyo kila kitu huwezi kujenga barabara kama wafanyabiashara hawataki kulipa kodi, huwezi kuimarisha huduma za afya kama hakuna kodi na pia huwezi kuimarisha mifumo ya elimu bila kodi," alisema Shigela.

Meneja wa TRA Mkoa wa Tanga, Specioza Owure, alisema maofisa hao wa TRA wanaofanya kampeni ya elimu kwa mlipakodi, watafika maeneo mbalimbali yenye wafanyabiashara katika mkoa wa Tanga na watawaelimisha kuhusu umuhimu wa kodi na kuwahamasisha kulipa kodi kwa wakati.

Alisema: "Maofisa wa TRA wanatumia jitihada zote kuwaelimisha wafanyabiashara, tunafanya hivi ili kila mmoja afahamu wajibu wake wa kulipa kodi sambamba na kusogeza huduma za TRA karibu na wateja."



Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Kawawa (wa tatu kulia), na Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Hassan Maajar Trust, Shariff Hassan Maajar (wa tatu kushoto), wakikata utepe wakati wa hafla ya kukabidhi msaada wa majengo ya vyoo kwa ajili ya Shule za Msingi za Nia Njema na Majengo zote za wilaya hiyo, ambao ulitolewa na taasisi hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Wadau wa lishe waombwa kutokomeza udumavu

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, Asia Abdallah, ametaka wadau wa lishe kupambana kutokomeza udumavu katika wilaya hiyo, ili kuwa na jamii bora isiyo na udumavu.

Akizungumza juzi wakati wa kikao cha tathmini ya lishe, alisema kuwa Wilaya ya Kilolo ni mmoja kati ya wilaya za mkoa wa Iringa ambazo hazina shida ya chakula, hivyo si sahihi wilaya hiyo ikawa na tatizo la udumavu wakati chakula kipo cha kutosha.

"Kwanini Kilolo tuendelee kuwa na udumavu wakati tunalima matunda ya kutosha, tuna wanga wa kutosha na mboga za majani za kutosha," alisema na kuongeza:

"Tuna kila aina ya virutubisho vya mwili, tumekuwa na changamoto ndogo ndogo ambazo zilikiukwa toka zamani ila sasa ni wakati mzuri wa kuzifanyia kazi changamoto hizo."

Alisema moja kati ya changamoto kubwa ni baadhi ya wazazi kutozingatia utunzaji mzuri wa watoto wakati wakiwa na ujauzito na baada ya ujauzito kwa kushindwa kulea watoto kwa kipindi cha siku 1,000 kama inavyotakiwa kwa mtoto kutunzwa.

Alisema kuwa suala lishe limekuwa na tatizo mtambuka katika Taifa na miongoni mwa mikoa yenye changamoto ya lishe ni Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Kilolo ikiwa ni miongoni, hivyo ni wajibu kwa wadau wote ndani ya wilaya hiyo kupambana na suala la lishe.

Alisema kuwa pamoja na kuwa hali ya lishe katika wilaya hiyo imezidi kusogea mbele ukilinganisha na miaka ya nyuma ila bado kasi inapaswa kuongezwa zaidi ili kuona jamii inatumia vema vyakula vinavyozalishwa katika wilaya hiyo kama sehemu ya kuongeza lishe bora kwa jamii.

Aidha, aliagiza halmashauri kutenga fedha kwa mujibu wa maelekezo ya Waziri wa TAMISEMI kwa ajili ya kusaidia mapambano dhidi ya lishe na fedha hizo ambazo ni chini ya shilingi 200 kwa kila mtoto zitolewe kwa wakati.

Ofisa Lishe wa Mkoa wa Iringa, Neema Mtekwa, alisema kuwa jamii imekuwa ikishindwa kutumia lishe yenye virutubishi hali inayosababisha kwa kiasi kikubwa kuwa na utapiamlo na udumavu.

Neema alisema kuwa kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka juzi kuhusu hali ya lishe nchini, mkoa wa Iringa una watoto 15,000 chini ya miaka mitano wenye udumavu, sawa na asilimia 47, huku kitaifa ikiwa na asilimia 31.8.

"Watoto wenye ukondefu ni 8,473 sawa na asilimia 3.7, huku kitaifa ni asilimia 3.8 na hali ya kuzaliwa na uzito pungufu ni asilimia 6.2 sawa na watoto 4,842 na kitaifa mkoa una asilimia 6.3," alisema Neema.

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI 6 WANAOKARIBIA MABAO 100 EPL UK. 12&13




# NANI MCHEZAJI BORA LIVERPOOL 2019/20?

**LIVERPOOL, England**

KIPIGO cha Manchester City cha 2-1 kutoka kwa Chelsea Alhamisi usiku kilishuhudia Liverpool ikinyakua ubingwa wa Ligi Kuu ya England.

Imemaliza ukame wa kusubiri miaka 30 kulipeleka kombe hilo katika Uwanja wa Anfield na Kocha, Jurgen Klopp amekuwa wa kwanza kwa kipindi cha miaka hiyo kulinyakua kombe hilo.

Kuwa mabingwa huku mechi saba zikiwa zimesalia, kumeifanya ligi hiyo kuwa ya upande wa Liverpool msimu huu.

Hivyo, kutokana na historia hiyo, wachezaji wengi wa Liverpool watajikuta wakitunukiwa tuzo binafsi mwishoni mwa msimu huu kwa mafanikio hayo.

Lakini ni mchezaji gani alikuwa shujaa kwa kikosi cha Klopp? Hapa tunawaangalia nyota kadhaa kutokana na viwango vyao dimbani.

**TRENT ALEXANDER-ARNOLD**

Trent Alexander-Arnold ametoa mchango wa aina yake kwa kikosi hiki, achana na Sadio Mane, Mohamed Salah na Roberto Firmino kama unaweza, halafu mtazame mchezaji huyu kinda, namna alivyokuwa akicheza katika nafasi yake ya ulinzi.

Akiwa ndio kwanza ana umri wa miaka 21, lakini amekuwa mmoja wa wachezaji waliotoa mchango mkubwa zaidi kwa Liverpool. Pia Alexander-Arnold alikuwa na pasi za mwisho 12.

**VIRGIL VAN DIJK**

Van Dijk amekuwa mmoja ya nguzo kuu ya Liverpool msimu huu, akianza kila mchezo wa Ligi Kuu England. Mholanzi huyo alicheza mechi 14 bila timu yake kuruhusu bao.

Uongozi wake kwa nafasi ya mlinzi wa kati uliisaidia sana Liverpool kupunguza mashambulizi langoni mwao.

**JORDAN HENDERSON**

Ikiwa Van Dijk ndiye Roll Royce nyuma na watatu wa mbele ni gari za michezo zenye uwezo wa kutoka spidi ya kilometa 0 hadi 60 kwa saa, basi Jordan Henderson anakwenda sambamba na spidi hiyo.

Chini ya Klopp, asilimia ya ushindi wa Liverpool ni karibu asilimia 13 ya juu (asilimia 68.8 ikilinganishwa na 56) wakati Henderson akicheza. Kipigo pekee kwenye ligi hadi sasa msimu huu, mbali na Watford ni pale walipocheza bila nahodha huyo.

Kiungo huyo amechangia pia kwenye ushambulizi, akitoa pasi za mwisho na kufunga mabao matatu msimu 2019/20. Henderson analijua jukumu lake la kucheza akiwa dimbani. Akiwa ameshanyakua taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, sasa amekuwa nahodha wakati Liverpool wakibeba taji la Ligi Kuu England.

**SADIO MANE**

Mara kwa mara wanasema kama unataka kuwa bingwa hakikisha unashinda wakati unapocheza vizuri. Wakati mwingine ushindi unakuwa mgumu kwa Liverpool na walikuwa wanahitaji mwokozi. Mara kwa mara, mwokozi wao amekuwa Sadio Mane.

Mane amekuwa mmoja wa washambuliaji muhimu zaidi kwa Liverpool kwa msimu wote na hadi sasa amefunga mabao 15 na kutoa pasi za mwisho saba. Mabao yake hayo yamekuwa msaada mkubwa kwa timu wakipata jumla ya pointi 18 msimu huu 2019/20. Wakati Liverpool walipokuwa na ukame wa mabao, Mane ndio alikuwa mkombozi wao.

**MOHAMED SALAH**

Salah alianza msimu wa kuvutia baada ya kuwasili hapo akitokea AS Roma na kufunga mabao 44 katika mashindano yote msimu wa 2017/18. Hata msimu uliopita raia huyo wa Misri alifunga mabao 22 kwenye Ligi Kuu England na pia msimu huu wa 2019/20 ndio mchezaji wa Liverpool anayeongoza kwa kuzifumania nyavu.

Ana jumla ya mabao 21 katika mashindano yote aliyocheza msimu huu, huku hakuna mchezaji wa Ligi Kuu England.

Hata hivyo, Salah sio tu mfungaji wa mabao, kwani pia ametengeneza nafasi za kufunga 49 na pasi za mwisho saba.

## ISIKUPITE

KENNY Dalglish ndiye alikuwa Kocha Mkuu wa Liverpool wakati timu hiyo ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu England kwa mara ya mwisho mwaka 1990. Mkongwe huyo alikuwa jukwaani peke yake kukitazama kikosi hicho kikitoa kichapo cha mabao 4-0 dhidi ya Crystal Palace wiki iliyopita.



## Extra Time



# WACHEZAJI 6 WANAOKARIBIA MABAO 100 EPL

**LONDON, England**

SUBIRA yavuta heri! Ndivyo unavyoweza kusema kwa Liverpool subira ya miaka 30 na kushinda taji la Ligi Kuu England imetimia baada ya Manchester City kupoteza mabao 2-1 dhidi ya Chelsea, hivyo kuwathibitisha Wekundu hao kuwa mabingwa wapya wa ligi hiyo msimu huu wa 2019/20.

Kikosi hicho cha Kocha, Jurgen Klopp kilihitaji ushindi mmoja ili kushinda kombe hilo, lakini baada ya Chelsea kuifunga City maana yake ni kwamba, Liverpool haiwezi tena kufikiwa pointi na timu yeyote ile katika msimamo wa ligi hiyo.

Ni kombe la 19 la Liverpool na lao la kwanza tangu msimu wa 1989/90.

Licha ya kutakiwa kusalia nyumbani na meya wa mji huo kutokana na virusi vya corona, maelfu wa mashabiki waliandamana hado kwenye Uwanja wa Anfiled kusherehekea ushindi huo.

Wengi wa mashabiki waliongozana katika uwanja wa klabu hiyo walivalia barakoa, huku wengine wakiwasha fataki.

Lakini wakati Liverpool ikitwaa ubingwa huo ni wachezaji 28 katika historia ya miaka 28 ya Ligi Kuu England, EPL, wamefunga mabao 100 kwenye mashindano hayo.

Makala hii tunawaangalia wachezaji sita ambao wamefunga mabao angalau 75 kwenye Ligi Kuu England na wana nafasi ya kufikisha 100 kwa siku zijazo.

**DANIEL STURRIDGE- MABAO 76**

Daniel Sturridge kwa sasa anatumikia adhabu ya kutocheza soka la ushindani sehemu yoyote duniani hadi mwezi ujao baada ya kupatikana na hatia ya kucheza michezo ya kubashiri matokeo ya mechi za soka.

Lakini mchezaji huyo wa zamani wa Liverpool, Chelsea na Manchester City ndio kwanza ana umri wa miaka 30, na anaweza kurudi kucheza kwenye Ligi Kuu England.

Wakati anafungiwa kucheza soka, Sturridge alikuwa na mkataba na timu ya Trabzonspor ya nchini Uturuki. Klabu ya katikati au ya chini inaweza kumsajili kwenye EPL na hivyo ana nafasi ya kuongeza mabao kwa siku za usoni.

RAHEEM STERLING- MABAO 78

Mshambuliaji, Raheem Sterling kwa sasa amekuwa na wakati mzuri wa kufunga mabao kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Sterling kwa kuwa umri wake sio mkubwa ana nafasi kubwa sana ya kufikisha mabao 100 katika siku chache zijazo.

**SADIO MANE- MABAO 80**

Tangu alipoanza kuichezea Southampton na sasa Liverpool, Sadio Mane kamwe hajawahi kushindwa kufunga mabao kwenye Ligi Kuu na hiyo ni tangu alipotua nchini England mwaka 2014.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Senegal, idadi kubwa ya mabao aliyofunga kwa msimu mmoja ni magoli 22, ambayo aliyapata kwenye msimu wa 2018/19 na kutunukiwa kiatu cha dhahabu. Na namna mambo yanavyokwenda, ana nafasi kubwa ya kufikisha mabao 100 kwenye Ligi Kuu England.

**OLIVIER GIROUD- MABAO 81**

Olivier Giroud amefunga mabao 12 ya Ligi Kuu England tangu kuanza msimu wa 2017/18, na hiyo yote ni kutokana na kutopata nafasi nyingi ya kucheza.

Raia huyu wa Ufaransa atabakia pale Chelsea kwa mwaka mwingine mmoja na pia atakabiliwa na ushindani pale Stamford Bridge hasa kutokana na ukweli kwamba -Timo Werner atawasili, na hivi karibuni atatimiza umri wa miaka 34. Nafasi yake ya kufikisha mabao 100 kwenye Ligi Kuu ni kubwa kama akiendelea kucheza.

**EDEN HAZARD- MABAO 85**

Eden Hazard kwa sasa hachezi kwenye Ligi Kuu England, lakini milango haijafungwa kwa nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, ambaye kwa sasa anakiwasha kule Real Madrid na anaweza kurudi kama mambo yanaendelea kutokuwa sawa kama ilivyo sasa.

Hazard aliondoka Chelsea akiwa na mabao 85 kwenye Ligi Kuu, na hivyo kama siku moja atarudi tena kwenye ligi hiyo, kiungo huyo ana nafasi kubwa ya kuongeza mengine na kufikisha mabao 100. Rekodi yake inaonyesha kwamba amekuwa akifunga kati ya mabao 14 na 16 kila msimu.


**JAMIE VARD - MABAO 99**

Jamie Vardy anaongoza kwenye mbio za kuwania kiatu cha dhahabu msimu huu 2019/20, bao lake moja (kabla ya mechi za mwishoni mwa wiki) linaweza kumfanya kuwa mchezaji wa 29 kufikisha mabao 100 kwenye ligi hiyo.

Historia ya Vardy inajulikana vizuri tu kutokana na uwezo wake wa kuzifumania nyavu. Kwa umri wake ana nafasi kubwa zaidi ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye ligi hiyo kwa siku za usoni.

## Nukuu

"Sasa nipo vizuri na ninachokifikiria ni Ligi ya Mabingwa Ulaya tu. Tuna kikosi imara na tumefuzu kibabe, hivyo tunasubiri tu shughuli ianze, nimekumbuka sana. Nasubiri kwa hamu kuingia uwanjani na kwa mapenzi ya Mungu, tutaandika historia." **Mshambuliaji wa PSG, Neymar alisema.**



"Klabu kama Real Madrid, Barcelona, Juventus, Manchester City, Manchester United na Liverpool zina historia kubwa kwenye soka na uwepo wao una maana kubwa sana, ni jambo la kuvutia kuwapo kwenye rada zao kama mchezaji, ni jambo zuri kwangu kwani itanifanya niongeze bidii uwanjani. Kucheza kwenye klabu hizi inabidi uwe na ubora mkubwa," **alisema Raul Jimenez, straika wa Wolves.**



"Sidhani kama mmemwona Eriksen wa ukweli. Naweza kuimarika zaidi na nina matumaini ya kufunga zaidi, nilifanya hivyo dhidi ya Napoli, lakini sikuweza kuisaidia timu. Lakini sasa naweza kusema ubora wangu unakuja na nitakuwa kwenye kiwango cha kuvutia, na nataka kuwa katika ubora wangu." **Straika wa Inter Milan, Dier Eriksen alisema alipokuwa akizungumza na Sky Sport.**



# 'HAT-TRICK' 7 ZAVUNJA REKODI MSIMU ULIOPITA

Na Mwandishi Wetu

MABAO matatu yaliyofungwa na straika wa Biashara United, Atupele Green, Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma, timu hiyo ikiichapa KMC ya Kinondoni mabao 4-0, kumeifanya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kufikisha 'hat-trick' saba na kuvunja rekodi ya msimu uliopita.

Msimu uliopita 2018/19, Ligi Kuu Tanzania Bara ilimalizika kukiwa na 'hat-trick' sita, ambazo zilifungwa.

'Hat-trick' sita za msimu uliopita zilipatikana kwa wachezaji Alex Kitenge wa Stand United, Emmanuel Okwi wa Simba aliyefunga 'hat-trick' mara mbili kwa msimu mmoja, Salum Aiyee wakati huo akiwa Mwadui, Fully Maganga wa Ruvu Shooting na Meddie Kagere wa Simba.

Atupele alipata mabao matatu 'hat-trick', kwenye dakika ya 69, 73 na 90 dhidi ya KMC na kuvunja rekodi hiyo ya msimu uliopita.

Hawa ni wachezaji waliofunga magoli matatu, 'hat-trick' saba msimu huu pamoja na mechi zake.

**1. Ditram Nchimbi (Polisi Tanzania 3-3 Yanga)**

Mchezaji wa kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu kufunga 'hat-trick' ni Ditram Nchimbi, wakati huo akichezea Polisi Tanzania, kabla hajahamia kwenye klabu ya Yanga kipindi cha dirisha dogo la usajili.

'Hat-trick' yake aliipiga kwenye mechi dhidi ya Yanga, Oktoba 2 mwaka jana zilipocheza kwenye mzunguko wa kwanza kwenye Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam na timu hizo kutoka sare ya mabao 3-3.

Ditram alifunga magoli hayo dakika ya 33, 55, na 57, huku ya Yanga yakifungwa na Mrisho Ngassa na David Molinga aliyefunga mawili.

**2. Daruwesh Saliboko (Lipuli 5-1 Singida United)**

Huyu ni straika wa Lipuli, ambaye ni mchezaji wa pili kufunga magoli matatu kwenye mechi moja msimu huu 'hat-trick'.

Ilikuwa ni Novemba 6 mwaka jana, alipofunga magoli hayo kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Singida United. Katika mechi hiyo Lipuli ilishinda mabao 5-1.

Alifunga kwenye dakika ya 43, 72 na 87, huku Paul Nonga akifunga mawili, Jonathan Daka, aliifungia Singida United bao la kufutia machozi.

**3. Obrey Chirwa (Azam 5-0 Alliance)**

Mzambia Obrey Chirwa ya Azam FC, naye msimu huu ameingia kwenye kitabu cha kumbukumbu, baada ya kufunga 'hat-trick' yake Novemba 25 mwaka jana kwenye Uwanja wa Nyamagana.

Ilikuwa ni dakika ya nne, 25 na 68, akiipa ushindi timu yake dhidi ya Alliance kwa mabao 5-0.

Mabao mengine ya Azam FC yalifungwa na Shaaban Chilunda, aliyefunga magoli mawili.

**4. Kelvin Sabato (Kagera Sugar 3-0 Singida United)**

Straika wa timu ya Kagera Sugar, Kelvin Sabato naye alifunga 'hat-trick' yake msimu huu kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba wakati timu yake ikicheza dhidi ya Singida United na kushinda mabao 3-0, Februari Mosi mwaka huu.

Magoli yote yalifungwa na Sabato, dakika ya 26, 88 na 90.

**5. David Richard (Alliance FC 4-1 Mwadui)**

Hata jina kubwa kwenye ulimwengu wa kandanda nchini, lakini ameingia kwenye rekodi ya kuwa mchezaji aliyefunga 'hat-trick' msimu huu.

Huyu ni David Richard ambaye ni straika wa Alliance. Yeye alifanya hivyo Februari 19 kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Mwadui kwenye Uwanja wa Nyamagana mjini Mwanza.

Alifunga dakika ya tatu, 18 na 83, goli lingine likifungwa na Sameer Vicent, Ottu Samuel akiifungia Mwadui bao la kufutia machozi.

**6. Meddie Kagere (Simba 8-0 Singida United)**

Mnyarwanda Meddie Kagere ndiye straika pekee ambaye amerejea tena kwenye orodha ya wafunga 'hat-trick' msimu huu, huku wenzie wa msimu uliopita wakiwa bado hajafanya hivyo.

Ilikuwa ni Machi 11 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam alipofunga 'hat-trick' kwenye mechi ambayo Simba iliifunga Singida United mabao 8-0.

Kagere aliyefunga magoli manne, aliyapata dakika ya kwanza, 25, 41 na 70.

Magoli mengine ya Simba yalifungwa na Deo Kanda aliyefunga mawili, John Bocco na Sharaf Shiboub.

**7. Atupele Green (Biashara United 4-0 KMC)**

Atupele alifunga magoli yake dakika ya 69, 73 na 90, akiisaidia timu yake ya Biashara United kushinda nyumbani mabao 4-0 dhidi ya KMC. Bao lingine ya Biashara lilifungwa na Justine Omari na kuwa 'hat-trick' ya saba msimu huu wa 2019/20 mpaka sasa.



KAGERE

**JE, WAJUA?**



MARA ya mwisho mchezaji wa Manchester United kufunga 'hat-trick kwenye Ligi Kuu England ilikuwa msimu wa 2012/13 kupitia mshambuliaji, Robin van Persie ambaye alifunga mabao matatu Aprili 22, mwaka 2013 ikiwa imepita michezo 263.

## Upinzani wawaita watu wenye ulemavu kugombea Oktoba

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VYAMA vya upinzani Mkoa wa Dodoma, vimewataka watu wenye ulemavu ambao wana sifa ya kuwa viongozi kuchangamkia fursa ya kujitokeza ya kugombea nafasi za ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Rai hiyo ilitolewa jana na viongozi wa vyama hivyo katika warsha ya kufanya ushawishi wa kuingiza masuala ya watu wenye ulemavu katika ilani zao za uchaguzi.

Akizungumza kwenye warsha hiyo, Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo Mkoa wa Dodoma, Yohana Mussa, alisema milango ipo wazi kwa watu wenye ulemavu kujitokeza kugombea nafasi hizo kwenye vyama hivyo na kuwaomba wajitokeze wale wote wenye sifa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa UPDP Mkoa wa Dodoma, Runna Kapya, alisema kuwa changamoto kubwa waliyonayo ya watu wenye ulemavu ni kutojiamini wenyewe na hata kama wana vigezo na sifa ya kujitokeza kuwania nafasi hizo ambazo ni muhimu kwa upande wao.

Awali, mwezeshaji wa warsha hiyo, Francis Mbisso, alivitaka vyama vya siasa kuacha tabia ya kuwashinikiza watu wenye ulemavu wawachague viongozi wanaowataka wao, badala watoe uhuru na haki ya kimsingi ya kuwachagua wanaowataka wenyewe.

Mbisso alisema kumchagua kiongozi ni gharama kubwa, hivyo wanawataka vyama vya siasa kuacha watu wenye ulemavu kuchagua viongozi wanaowataka wenyewe na siyo kuchaguliwa kama ilivyozoeleka kwenye uchaguzi uliopita.

Naye, Askofu Frank Laurent wa Kanisa la Viziwi la Bethel Baptist Deaf Church of Tanzania (BBDCT), akizungumza kwenye warsha hiyo iliyodhaminiwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Foundation for Civil Society, aliiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuandaa mazingira bora ya uchaguzi kwa watu wenye ulemavu kutokana na jamii ya watu wenye ulemavu wa aina yote wamekuwa wakisahauliwa kushiriki kwenye mchakato wa uchaguzi wa ngazi mbalimbali.

Laurent alisema watu hao wamekuwa wakikosa haki yao ya kimsingi ya kushiriki katika ushindani wa kugombea nafasi mbalimbali ya uongozi kwa kuwa wanasifa za kuwa viongozi.

# Madereva waliotumbuliwa kwa vyeti feki wamwangukia JPM

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MADEREVA 71 walioondolewa katika sakata la vyeti feki, wamemwomba Rais John Magufuli msamaha na kuwarejesha kazini baada ya kukidhi vigezo vinavyotakiwa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, msemaji wa umoja wa madereva hao, Rajab Mashashi, alisema baada ya serikali kuwaondoa katika nafasi zao kutokana na kutokuwa na sifa waliamua kujiendeleza ili kukidhi sifa walizozikosa ikiwamo kuwa na cheti cha kidato cha nne.

Alisema madereva hao ni miongoni mwa wafanyakazi walioondolewa katika ajira zao serikalini, kati ya mwaka 2016-2017 kwa kukosa sifa za msingi katika utumishi wa umma kwa kughushi vyeti vya kidato cha nne.

"Baada ya kuondolewa katika ajira tuliamua kuanzisha umoja wetu mwaka 2017 kwa ajili ya kupeana taarifa mbalimbali," ambapo waliamua kuhamasishana kujiendeleza kielimu.

Msemaji huyo alisema madereva 71 wanaomba msamaha kwa Rais na kurejeshwa kazini kwa kuwa wamejiendeleza kielimu kwa kufanya mtihani wa maarifa (QT) katika Shule ya Dodoma Sekondari kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

"Tumejiendeleza katika maeneo mbalimbali mfano mimi na Katibu wetu Geophrey Mangosongo tumejiendeleza kwa kusoma mwaka mmoja vidato viwili hapa Dodoma, kati ya hao wapo ambao wameshapa vyeti, wapo wanaosubiria vyeti vitoke na ambao bado wanaendelea na shule," alisema Mashashi.

Mashashi alisema wanajutia kitendo walichokifanya cha kughushi vyeti vya kidato cha nne licha ya kuwa walifanya hivyo kwa nia njema ya kujipatia ajira ili kuendesha maisha yao pamoja na kutoa mchango katika ujenzi wa Taifa.

"Tunamwomba msamaha Rais John Magufuli kwa kosa tulilolifanya wakati tunaomba kuingia katika ajira, tulikuwa zaidi ya 800 ambao tulipoteza ajira, tunawategemezi na maisha yetu yamekuwa magumu tangu tulivyoondolewa kwenye ajira," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa sasa wana sifa zote zinazostahili kupata ajira katika utumishi wa umma kama sheria za utumishi zinavyotaka.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa umoja huo, Gwaza Sonyo, aliahidi kuwa waaminifu katika kazi zao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma, pamoja na sheria za usalama barabarani.



Mwenyekiti wa Wanawake Wajane wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Jimbo la Dodoma, Shile Sheshu, akizungumza na wajane (hawapo pichani) kwenye maadhimisho ya Siku ya Wajane yaliyofanyika jana, makao makuu ya kanisa hilo, jijini Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**.

# Masoko ya Dodoma kuboreshwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amepania kuyafanya masoko ya Jiji la Dodoma kuwa na hadhi ya makao makuu ya nchi ili wafanyabiashara wapange bidhaa zao kwenye mazingira rafiki.

Mavunde ambaye ni Mbunge wa Dodoma Mjini, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akikabidhi mabati na nguzo za chuma za kuezeka paa la soko la matunda na mboga Bonanza jijini humo, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa katika uchaguzi mwaka 2015.

Mavunde alisema kuboreshwa kwa miundombinu ya masoko ya jiji hilo ni kuunga mkono jitihada za Rais John Magufuli za kuhamishia Makao Makuu Dodoma.

Alisema utekelezaji wa ahadi hiyo ulitokana na ombi la wafanyabiashara kujengewa paa kwa kuwa walishindwa kupanga bidhaa zao msimu wa mvua na kuharibiwa na jua.

"Kutokuwapo kwa paa katika soko hili kumechangia wafanyabiashara wengi kutoingia kwenye soko hili kwa sababu hawawezi kuweka bidhaa zake hapa katikati kwenye mvua na jua kwa hiyo mwisho wa siku eneo liliachwa wazi bila kutumika," alisema.

Alisema soko hilo ni miongoni mwa masoko ambayo ameendelea kuyaboresha ili wafanyabiashara wafanye biashara zao kwenye mazingira rafiki.

"Nilipokea ombi lenu, mimi dhamira yangu ni kuwatumikia watu na kuwasaidia kufikia maendeleo yao, leo nimeleta vitu vyote vya muhimu vya kuezeka paa kwa asilimia 80, ambapo kuna mabati 400 na nguzo za chuma 100 vyenye thamani ya shilingi milioni 25, vimebaki vidogo ambavyo tutakamilisha ili liwekwe paa," alisema.

Alisema anataka masoko hayo yawe na hadhi ya makao makuu na wafanyabiashara wafanye kwenye mazingira mazuri.

"Kazi inayofanyika ni kuishi kwa vitendo kwa kazi anayoifanya Rais Magufuli, soko hili litakuwa na meza zote zinazofanana na za kisasa za chuma ili kulifanya soko lipendeze," alisema.






Meneja Mkuu wa Kiwanda cha TBL Mbeya, Fabian Godwin (kulia), akimwelezea Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, na ujumbe wake juu ya kiwanda hicho kinavyozalisha bidhaa zake alipofanya ziara ya kikazi mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Rujewa yalalamika kukosa majisafi

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

BAADHI ya wakazi wa Mji wa Rujewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali wanadaiwa kuwa wanalazimika kuhatarisha maisha yao kwa kunywa maji ya kwenye mifereji ya umwagiliaji wa mpunga na baadhi kuchimba kwenye mchanga kutokana na mji huo kukosa huduma ya majisafi ya bomba.

Wananchi wanaoathirika zaidi na tatizo hilo ni wa Kitongoji cha Mayota, ambao wanadai wanatumia maji yaliyochanganyika na tope hali ambayo inahatarisha afya zao kutokana na kuwa katika hatari ya kupata magonjwa ya mlipuko.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mayota, Ezekiel Njuguya, alisema tatizo la ukosefu wa maji ni la muda mrefu na linawasababishia wananchi matatizo makubwa.

Aliiomba serikali kufanya utaratibu wa kuwapelekea wananchi wake mradi wa maji ili waondokane na tatizo hilo ambalo linahatarisha maisha yao ikiwamo kusababisha ugonjwa wa kipindupindu na maradhi ya matumbo.

"Wananchi wangu, wanalazimika kunywa maji yaliyochanganyikana na tope hasa wakati wa kiangazi, tunaiomba serikali iliangalie hili jambo, ili kuwanusuru wananchi wangu kwa kuwapatia huduma ya majisafi na salama, tatizo hili ni la muda mrefu sana," alisema Mayota.

Alisema kuwa kitongoji hicho hakina huduma ya maji ya bomba wala kisima kwa zaidi ya miaka 10, hali ambayo inawafanya wananchi kutumia muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya shughuli za uzalishaji mali.

Naye Yazidu Abdul, mkazi wa Mtaa wa Kaniyonga, alisema licha ya kukosekana kwa huduma ya maji katika mtaa wao, lakini Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika mji huo (RUWASA) imekuwa ikiwatoza wananchi Sh. 5,000 kila mwezi kwa ajili ya huduma ya maji.

Alisema eneo hilo lilianza kukosa huduma ya maji wakati barabara ya Rujewa-Ubaruku ilipokuwa inajengwa kwa kiwango cha lami, lakini wananchi waliendelea kutozwa kiasi hicho cha fedha jambo ambalo alisema ni kuwanyonya.

Kwa upande wake Kaimu Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Rujewa, Tuntufye Chamba, alisema atawasilisha masuala yote yanayohusu matatizo ya upatikanaji kwa uongozi wa RUWASA kwa kuwa wao ndio wenye jukumu la kusimamia usambazaji wa maji.

"Meneja wa RUWASA kwa bahati mbaya hayupo leo, lakini yote haya nimeyapokea na nitamfikishia malalamiko haya ili ayashughulikie na nitahakikisha mnapata mrejesho haraka, tatizo la maji kwenye maeneo mengine sasa hivi limebaki historia," alisema Chamba.

Alisema kuna fedha zimepelekwa na baadhi ya washirika wa maendeleo katika mji huo kwa ajili ya kuwachimbia wananchi visima vya maji, na kwamba atahakikisha kitongoji cha Mayota kinakuwa miongoni mwa maeneo yatakayonufaika na mradi huo.

Mwaka 2016 Mji wa Rujewa ni miongoni mwa maeneo katika Mkoa wa Mbeya ambayo yalikumbwa na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu kutokana na wananchi wake kutumia maji machafu.

# RC asisitiza Polisi kusimamia utaratibu wa magari kupishana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amelisisitizia Jeshi la Polisi mkoani humo kuendelea na utaratibu wa kuzuia magari ya abiria na mizigo kupishana kwenye maeneo yenye miteremko mikali ili kuepusha ajali za barabarani.

Chalamila alitoa msisitizo huo juzi jioni kupitia mitandao alipokuwa anatoa salamu za pole kwa wananchi wa Mkoa wa Iringa kufuatia ajali ya basi iliyotokea katika mteremko wa Mlima Kitonga ambayo iligharimu maisha ya watu kadhaa na wengine kujeruhiwa.

Alisema katika Mkoa wa Mbeya baada ya ajali za barabarani kukithiri hasa kwenye maeneo ya milima, Kamati ya Ulinzi na Usalama ilichukua hatua kadhaa ikiwamo kuyasimamisha magari ya mizigo kabla hayajaanza kuteremka kwenye milima ili kuyakagua mifumo yake ya breki.

Alisema magari ya abiria na ya mizigo yanapita kwa awamu katika maeneo yote ya miteremko kwa maelezo kuwa utaratibu huo unasaidia kupunguza madhara kwa binadamu endapo ajali itatokea.

"Nampa pole sana Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, Jeshi la Polisi mkoani humo pamoja na wananchi wote wa Mkoa wa Iringa kwa kuwapoteza wapendwa wetu katika ajali hiyo na ninawaombea majeruhi wapone na waendelee kufanya shughuli za maendeleo," alisema Chalamila.

Aidha, alisema alisikitika baada ya kuona wengi waliopoteza maisha kwenye ajali hiyo walikuwa ni watoto wadogo ambao walikuwa wanasafiri na wazazi wao.

Aliwataka wazazi waliowapoteza watoto wao kwenye ajali hiyo kuwa wavumilivu katika kipindi hiki kigumu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila ni mzaliwa wa Mkoa wa Iringa na kabla ya kuteuliwa na Rais kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, alikuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika mkoa huo.

# NMB yasaidia elimu, afya mil. 25/- Mbeya, Songwe

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeendelea kutimiza ahadi yake ya kurudisha faida kwa jamii baada ya kutumia Sh. milioni 25 katika misaada kwenye elimu na afya mikoa ya Songwe na Mbeya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na benki hiyo jana, sehemu ya msaada huo ni madawati kwa ajili ya shule wilayani Momba na mabati ya Hospitali Teule ya Rufani Vwawa mkoani humo.

Akizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa kukabidhi msaada huo Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Straton Chilongola, alisema wameamua kutoa msaada huo baada ya kupokea maombi ya uhitaji kwenye eneo la elimu na afya.

Akiwa eneo la Shule ya Msingi Nzoka, Chilongola, alisema benki hiyo imetoa jumla ya madawati 53 na pia mabati 174 baada ya kupokea maombi ya uhitaji, vitu vyote hivi ambavyo kwa ujumla vina gharama ya Sh. milioni 10.

Mkuu wa Wilaya ya Momba mkoani humo, Juma Irando, alieleza kuwa NMB wamekuwa wadau wakubwa katika kutoa misaada mbalimbali ya kijamii.

"Wilaya ya Momba tunayo bahati ya kupewa misaada kwenye eneo la maendeleo, benki ya NMB imekuwa ikitoa huduma bora na ushirikiano mzuri na serikali hususani katika maendeleo," alisema Mkuu huyo wa wilaya na kuongeza: "Hivyo, msaada huu wa madawati unatuma ujumbe kwa wanafunzi wahakikishe wanasoma kwa bidii."

Juma Mtengu ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Nzoka, ametoa shukrani za dhati kwa benki ya NMB na ameiomba benki hiyo iendelee kutoa msaada pindi wanapohitaji. Naye mwanafunzi wa shule hiyo, Gasto Josefu, ameishukuru benki ya NMB kwani idadi kubwa ya wanafunzi walikuwa wanakaa chini, hivyo kupitia msaada wa madawati waliyowapa itasaidia kupunguza wimbi la upungufu wa madawati katika shule hiyo.

Wakati huo huo, katika Hospitali Teule ya Rufani ya Vwawa mkoani humo benki ya NMB imetoa bati 174 zenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa ajili ya maboresho ya utanuzi wa jengo la wazazi na ujenzi wa sehemu ya kupumzikia wagonjwa na ndugu wanaokwenda kuwaona wagonjwa.

Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Lukombodzo Lulandala, wakati wa kupokea bati za msaada zilizokabidhiwa na Chilongola, alisema hospitali hiyo inahitaji jengo la wazazi na pia kuna ukosefu wa sehemu ya kupumzikia wagonjwa na ndugu wa wagonjwa.





# Mwanamke wa nne achukua fomu urais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, amekuwa mwanamke wa nne kujitokeza kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar.

Mgeni anakuwa mgombea wa 31 waliojitokeza kuchukua fomu kwa Chama Cha Mapinduzi kugombea nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhiwa fomu hiyo na Katibu wa Idara ya Oganaizesheni, Galos Nyimbo, alikishukuru chama kwa kutoa fursa hiyo kwa wanachama wake kuweza kugombea nafasi mbalimbali ikiwamo ya urais.

Alisema ataungana na wagombea wengine ambao tayari wameshachukua fomu, ambapo ni demokrasia ambayo imetoka kwenye chama na fursa kama mwanamke kutekeleza ilani ya uchaguzi ya 2015/2020 kuelekea 50 kwa 50.

Mgeni ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Baraza la Wawakilishi (UWAWAZA), alisema amehamasika kuchukua fomu hiyo kutokana na idadi ndogo ukilinganisha na wanaume.

Alisema imani yake ni kuwa, wanawake wengine watahamasika kuchukua fomu, ili kutekeleza haki yao ya msingi ya kuchaguliwa na kuiamini CCM ambayo ina nia njema na wanawake.

Alieleza kuwa yeye ni mwanaharakati ambaye amekuwa akihamasisha wanawake katika masuala mbalimbali yanayohusiana na haki zao za kisiasa.

Aliwapongeza wanawake wenzake ambao tayari wameshachukua fomu za kutia nia ya kugombea nafasi hiyo kwani wameonyesha ujasiri na kutumia demokrasia iliyokuwapo ndani ya CCM.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa Chama cha AFP, Said Soud Said, amechukuwa fomu ya kugombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya chama hicho huku akiahidi kufuata nyayo za Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Karume, kwa kuendelea kutoa huduma muhimu za kijamii ikiwamo elimu, matibabu na maji safi bure.

Soud aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Ali Mohamed Shein, kwa uongozi bora wenye busara.

"Nachukuwa fomu ya kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kuwa mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha AFP... nikichaguliwa huduma zote muhimu za kijamii ni bure ikiwamo elimu, matibabu na majisafi na salama," alisema.

Akikabidhi fomu hizo, Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Omar Juma, alisema mgombea anatakiwa kutafuta wadhamini 150 katika mikoa ya Zanzibar ikiwamo Pemba.



Mwenyekiti wa Chama cha AFP, Said Soud (kulia), akipokea fomu ya kugombea urais wa Zanzibar kupitia chama hicho. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Waziri ataka ushiriki wazawa kukuza elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema sekta ya elimu itaendelea kukua kwa kushirikiana na wazalendo mbalimbali nchini.

Akizungumza katika hafla ya kufungua darasa katika Shule ya Msingi na Sekondari ya Kidimni wilayani Kati Mkoa wa Kusini Unguja, alisema ili Taifa lifike katika uchumi wa kati ipo haja ya kusimamia elimu ipasavyo ili nchi iendelee kupata wataalamu mbalimbali nchini.

Aidha, aliwataka wazazi kuhakikisha wanatimiza wajibu wao katika malezi ya watoto ili kuepukana na vitendo viovu vya udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia.

Pia, Pembe aliwataka wazazi kushirikiana na walimu kwa kuwasaidia masomo watoto wao wanapokuwa nyumbani ili waweze kufaulu na kufikia malengo yao.

Waziri huyo aliwataka walimu kutimiza majukumu yao ili wanafunzi waweze kupata elimu bora hasa kwa kuziba mapengo kipindi walichokosa masomo kwa kufungwa shule kutokana na mlipuko wa maradhi ya corona.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Mohamed Raza, alisema kiongozi mzuri ni aliye mzalendo mwenye kuleta maendeleo yanayowafaa watu wote hasa katika sekta ya elimu.

Akisoma risala kwa niaba ya walimu wenzake, Rahma Muombwa, alisema shule ina upungufu wa madarasa kutokana na wingi wa wanafunzi.

Aidha, aliiomba Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na mwakilishi wao kusimamia ujenzi wa bwalo la shule pamoja na uzio ili kupunguza uharibifu unaotokana na wanyama wanaofugwa karibu na shule

# ZEC yazindua Kamati Maadili ya Uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), imezindua Kamati ya Maadili ya Uchaguzi Mkuu ambayo itakuwa na jukumu la kuandaa kanuni za maadili ya kuongoza shughuli za vyama na wadau wengine.

Aidha, kamati hiyo inapaswa kufanyakazi kwa kushirikiana na tume kwa kushauriana na vyama vya siasa, msajili wa vyama vya siasa na mamlaka ya serikali.

Akizungumza katika mkutano wa uzinduzi wa kamati hiyo, Makamu Mwenyekiti ZEC, Mabruki Jabu Makame, aliwataka wajumbe wa kamati hiyo kupanga mipango mizuri kulingana na sheria zilizopo katika kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa mafanikio makubwa.

Mabruki alisema kuwa, Tume ya Uchaguzi ina imani kuwa wananchi watayafuata maelekezo ya vyama vyao endapo kila mjumbe wa kamati hiyo atawajibika ipasavyo katika kutekeleza wajibu wake.

Alieleza kuwa kamati hiyo ni miongoni mwa kamati sita zilizoundwa na ZEC ili kupata ushauri juu ya masuala mbalimbali katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Naye Mkurugenzi wa Uchaguzi wa ZEC, Thabit Idarous Faina, alizitaja kamati hizo ambazo ni pamoja na kamati ya fedha, ununuzi na usambazaji wa vifaa, kamati ya elimu ya wapigakura, kamati ya ulinzi, usalama na vyombo vya dola, kamati ya mawasiliano na vyombo vya habari na kamati ya kuratibu shughuli za waangalizi wa uchaguzi.

Mkurugenzi huyo alieleza kuwa, miongoni mwa majukumu ya kamati hiyo ni kuandaa kanuni za uchaguzi pamoja na kuzisimamia ili kila mdau aweze kupata haki yake ya kushiriki katika uchaguzi ulio huru, haki na uwazi.

Aidha, alisema kuwa wajumbe wa kamati za ushauri katika uchaguzi mkuu ni washauri wazuri wa tume katika kuendesha uchaguzi unaozingatia misingi ya kidemokrasia kwa kila mwananchi.

Alifafanua kuwa, Kamati ya Maadili ya Uchaguzi imeundwa na wajumbe wanaowakilisha vyama vya siasa, ZEC, mjumbe kutoka serikalini, Jeshi la Polisi na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwa upande wa Ofisi ya Zanzibar.

Kwa upande wake Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hassan Nassir Ali, aliwaomba wananchi kuondoa hofu katika kipindi cha uchaguzi na kuwaomba viongozi wa vyama vya siasa ambao ni wajumbe wa kamati ya maadili kutii viapo vyao katika kamati hiyo na kufuata yale wanayoelekezwa katika kanuni za maadili ya uchaguzi.

Naye Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa kwa upande wa Zanzibar, Muhammed Ali Ahmedi, alivitaka vyama vya siasa ambavyo vimeshiriki katika kamati hiyo kuwa mstari wa mbele kusimamia kanuni za maadili ya uchaguzi, kuzilinda na kuzitangaza kwa wananchi, viongozi wenzao wa vyama vya siasa pamoja na vyombo vya dola.

## Masauni aahidi utatuzi makazi ya askari

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI iko mbioni kumaliza changamoto za makazi ya askari nchi nzima kwa Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uhamiaji.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliyasema hayo visiwani Pemba, baada ya kukagua nyumba 14 kati ya nyumba 400 zilizopo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Nyumba hizo zilighariimu zaidi ya Sh. bilioni 10 zilizotolewa na Rais Dk. John Magufuli, Aprili 2018, mkoani Arusha wakati wa kumbukumbu ya hayati Abeid Amani Karume.

"Serikali inatambua changamoto za makazi ya askari, na ujenzi wa nyumba hizo 400 ulishaanza nchi nzima na nyingine zishakamilika, napenda kuwaahidi askari wetu changamoto hiyo ya makazi itakuwa historia ndani ya muda mfupi, nimetembea baadhi ya mikoa nimeona jinsi askari wetu wanavyoishi," alisema Masauni na kuongeza:

"Baadhi ya mikoa tumeshajenga nyumba ikiwamo nyumba za askari Magereza Ukonga, nyumba za Uhamiaji Iyumbu Dodoma, nyumba za Polisi Medeli, Dodoma na mikoa yote nchini kuna nyumba ambazo askari wetu washaanza kukaa," alibainisha.

## Asasi yataka waraibu kusaidiwa kiuchumi

Na Beatrice Shayo

ASASI isiyo ya kiserikali ya Yovaribe imeomba kupatiwa wafadhili ambao watawawezesha vijana walioacha kutumia dawa za kulevya kujiendeleza kiuchumi, ili wasirudi katika matumizi ya dawa hizo.

Mtunza Takwimu katika mradi wa ubadilishaji wa sindano na mabomba kutoka Yovaribe, Jasmin George, alisema wakipatikana wafadhili kwa ajili ya kuwainua kiuchumi itawasaidia kukua kiuchumi kwani kuna baadhi yao wana elimu nzuri.

"Kumbuka huyu mpaka kuacha dawa hizo kazi yake ilikuwa ni kukaba ama kuokota chupa walikuwa wanafanya vitu ambavyo havikubaliki katika jamii, sasa umempa Methadone na elimu amejitambua lakini hujamuwezesha kiuchumi ili asirudi kule alikotoka," alibainisha George.

Aliongezea kuwa "Sisi tunatamani tupate wafadhili ambao watawasaidia kuanzisha miradi midogo midogo ya kuwakwamua kiuchumi, ili wao waweze kujitegemea wao wenyewe wasirudi tena kuwa tegemezi katika familia."

Aidha, alisema tangu kuanzisha kwa asasi yao zaidi ya watu 1,000 wamepona na wengine wanaendelea na utumiaji wa dawa za Methadone.

Aidha, alisema kumekuwa na uelewa mdogo kwa wananchi wanapokuwa wanatoa mabomba kwa watumiaji wa dawa za kulevya na kuonekana kama wanachochea matumizi hayo jambo ambalo sio la kweli.

# Mwanamke auawa kwa kupigwa mawe kisa tuhuma za ushirikina

Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linawasaka watu wasiojulikana kwa tuhuma za kumuua kwa kumpiga mawe, mwanamke aliyefahamika kwa jina la Maria Birika (40), mkazi wa Kijiji cha Myunga, Kata ya Mkali, wilayani Kalambo.

Imeelezwa kuwa watu hao wamemfanyia kitendo hicho kwa kumtuhumu kujihusisha na vitendo vya kishirikina.

Tukio la mauaji ya mwanamke huyo lilitokea Juni 26, saa 12:00 jioni baada ya watu hao kufika nyumbani kwake na kumkuta mtoto aliyefahamika kwa jina Given Lameck (15), akiwa amefungiwa nyumbani kwa mwanamke huyo, huku akiwa amefungwa kitambaa chekundu usoni.

Kabla ya mauaji hayo, mtoto Given alipotea nyumbani kwao katika mazingira ya kutatanisha, ndipo harakati za kumtafuta zilianza, na kwamba ndugu zake walimtafuta kwa muda mrefu bila mafanikio.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justine Masejo, alisema baada ya jitihada za kumpata mtoto huyo kushindikana, waliamua kutoa taarifa kwa uongozi wa kijiji kisha kuendelea kumtafuta.

Alisema baada ya kumtafuta kwa muda mrefu walifanikiwa kumkuta nyumbani kwa mwanamke huyo akiwa amefungiwa ndani na amefungwa kitambaa chekundu usoni, huku akionekana kana kwamba amechanganyikiwa kutokana na kuongea vitu visivyoeleweka.

Baada ya kupatikana kwa mtoto huyo, ndipo watu waliokuwa wakimtafuta walipo hamaki na kushikwa na hasira na kuanza kumpiga mwanamke huyo kwa mawe na vipande vya matofali vilivyokuwa karibu na nyumba yake na kumsababishia majeraha makubwa, kuvuja damu nyingi na kufariki dunia kutokana na kukosa matibabu ya haraka.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, akiongozana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Kamishna Msaidizi Makarani Ahmed (kushoto), baada ya ukaguzi wa makazi ya nyumba 14 za askari polisi (pichani) zilizojengwa baada ya Sh. bilioni 10 kutolewa na Rais John Magufuli kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 400 nchi nzima kutataua changamoto za makazi ya askari. **PICHA: WMN**

# Foleni Dar ilivyotesa wananchi

Na Elizabeth Zaya

WAKAZI wa Jiji la Dar es Salaam, wanaotumia barabara ya Bagamoyo juzi walikumbana na adha ya usafiri kwa kujikuta wanatumia saa nyingi barabarani na wengine kulazimika kutembea kwa miguui.

Foleni hiyo ilianza asubuhi mpaka usiku katika barabara nyingi za kuingia na kutoka jijini humo, huku kukiwa na idadi kubwa ya magari ya watu binafsi.

Kwa mujibu wa wakazi wa barabara hiyo, foleni hiyo ilisababishwa na wazazi wengi kusafirisha watoto wao kuwapeleka shuleni kwa ajili ya maandalizi ya kufungua leo.

Katika barabara hiyo, eneo ambalo gari nyingi zilionekana kukwama zaidi ni kuanzia Tegeta Kibo ambako gari zilionekana kusimama kwa muda mrefu bila kusogea mbele.

Foleni hiyo ilikuwa ikitembea kidogo sana baada ya kusimama eneo moja

kwa muda mrefu na ilionekana hivyo hadi kuelekea Bagamoyo nje ya Jiji la Dar es Salaam.

Kutokana na changamoto, wakazi wengi wa eneo hilo walionekana kutembea kwa miguu, na wengine wakitumia bodaboda.

Baadhi ya madereva wa gari binafsi walionekana kuamua kusimama kwa muda pembezoni mwa barabara na wengine wakiingia katika maduka ya vinywaji na sehemu za kuuza chakula kupata huduma kwanza kusubiri foleni ipungue.

Changamoto hiyo ya foleni ilikuwa katika sehemu zote mbili za barabara ya gari zilizokuwa zikielekea Bagamoyo pamoja na zile zilizokuwa zikitoka Bagamoyo kuingia Dar es Salaam.

Barabara nyingine ni ya Morogoro ambako kuna ujenzi, magari mchanganyiko mengi yakiwa malori yalitumia zaidi ya saa nne bila kusogea, na licha polisi wa kikosi cha Usalama Barabarani kuwapo lakini alishindwa kuyadhibiti.

Baadhi ya watumiaji wa barabara hiyo walisikika wakilalamika kwamba hawajawahi kukumbana na foleni ya namna hiyo ambayo haisababishwi na ajali.

## HABARI KIMATAIFA

## EU yakosa mwafaka kuondoa 'lock down' kwa wageni

**BRUSSELS, Ubelgiji**

MATAIFA ya Umoja wa Ulaya jana yalishindwa kufikia makubaliano juu ya orodha ya nchi zilizo salama ambazo raia wake wangeweza kuruhusiwa kuanza kusafiri ndani na nje ya kanda hiyo kuanzia Julai.

Mabalozi wa nchi 27 wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU) walikutana mjini Brussels jana kutayarisha mwongozo wa kuruhusu baadhi ya raia wa mataifa kadhaa duniani kuanza kuingia tena kwenye mataifa ya kanda hiyo bila ya masharti ya kukaa karantini.

Hata hivyo, wanadiplomasia hao wameomba muda zaidi wa kushauriana na serikali za mataifa yao kabla ya kufikia uamuzi wa orodha ya nchi 10 hadi 20 zilizopendekezwa na uamuzi unaotarajiwa kutolewa muda wowote.

Taarifa zaidi kutoka mjini Brussels zimesema orodha ya mataifa iliyowasilishwa kwa mabalozi hao haikuzijumuisha Marekani, Brazil wala Urusi, nchi ambazo bado zina kiwango kikubwa cha maambukizi ya virusi vya corona.

Kulingana na maofisa wawili wa Marekani, abiria kutoka Marekani wataruhusiwa kusafiri ikiwa watatimiza masharti kadhaa ikiwamo kupita katika vituo vya ukaguzi wa joto la mwili.

Halmashauri Kuu ya EU ilitoa ushauri kwa kanda hiyo kuondoa kwanza vizuizi vya mipaka ya ndani na kisha baadaye kuanza kufungua milango kwa wageni kutoka nje ya kanda hiyo.

Hata hivyo, hatua ya kwanza haikufanikiwa kama ilivyoainishwa kwenye mpango.

Ugiriki inawalazimisha wageni wote kutoka mataifa kadhaa ya kanda ya EU kufanyiwa vipimo vya ugonjwa wa corona na kujiweka karantini hadi matokeo yatakapotolewa.

Jamhuri ya Czech imesema haitoruhusu watalii kutoka Ureno, Sweden na sehemu zinginezo za Poland kuingia nchini humo.

Kwa sehemu kubwa mataifa ya kanda hiyo yanakubaliana kuwa yanapaswa kuruhusu wageni kutoka mataifa yenye viwango sawa au vizuri zaidi vya mafanikio ya kudhibiti ugonjwa wa corona.

**DW**

# Urusi yakana kuwalipa mgambo wa Taliban kuivamia Marekani

**MOSCOW, Urusi**

URUSI imekanusha madai kwamba ilikubali kutoa zawadi kwa wanamgambo wanaohusishwa na kundi la Taliban kuua vikosi vya Marekani na vingine katika muungano wa Nato nchini Afghanistan.

Gazeti la The New York Times na la Washington Post yaliwanukuu maofisa waliosema kuwa kitengo cha kijajusi cha Urusi kilichohusika na majaribio ya mauaji Ulaya mwaka jana kilikuwa kimejitolea kutoa zawadi.

Ubalozi wa Urusi nchini Marekani ulisema kwamba madai hayo yamesababisha wanadiplomasia kupokea vitisho.

Kundi la Taliban lilikanusha kwamba kulikuwa na makubaliano kama hayo na kitengo cha ujasusi cha Urusi.

Taarifa hizo zimetolewa wakati Marekani ikijaribu kufanya mazungumzo ya makubaliano ya amani kumaliza vita vya Afghanistan vilivyodumu kwa miaka 19.

Kulingana na gazeti la New York Times, Rais wa Marekani, Donald Trump aliarifiwa kuhusu taarifa hizo Machi, mwaka huu, lakini Ikulu ya Marekani imekanusha madai hayo.

"Siyo rais wala naibu wake, hakuna aliyearifiwa kuhusu madai yanayosemekana kutekelezwa na Urusi," alisema Kayleigh McEnany, ambaye ni Msemaji wa Ikulu.

Aliongeza kuwa: "Hili siyo kwa misingi ya madai yanayosemekana ila kwa ukosefu wa usahihi wa taarifa za gazeti la New York Times ambalo linaangazia taarifa ya uongo kuwa Rais Trump aliarifiwa kuhusu suala hilo."

Ofisa ambaye hakutajwa jina lake, aliyenukuliwa na gazeti la New York Times akisema kuwa idara ya ujasusi ya Marekani ilihitimisha miezi kadhaa iliyopita kwamba kitengo cha ujasusi cha Urusi kilikuwa kinatafuta kuyumbisha wapinzani wake kisiri kwa kujitolea kutoa zawadi kwa mashambulizi yatakayofanikiwa dhidi ya muungano wa vikosi vya Nato.

Wanamgambo wa Kiislamu au makundi ya uhalifu yalioaminiwa kuwa na uhusiano nao, inasemekana kwamba yalikuwa yamepokea pesa, gazeti hilo limesema.

Ujumbe kwenye mtandao wa Twitter, ubalozi wa Urusi nchini Marekani ulishutumu gazeti hilo kwa kueneza taarifa za uongo.

Maofisa walionukuliwa na gazeti la New York Times walisema kuwa Baraza la Usalama wa Taifa Ikulu, lilikuwa linatafakari namna ya kujibu madai hayo ikiwamo kuiwekea Urusi vikwazo vikali.

Inasemekana kwamba kitengo cha ujasusi cha Urusi pia kilikuwa kimehusishwa na jaribio la kuumua aliyekuwa jasusi wa Urusi, Sergei Skripal, na binti yake Yulia kwa kutumia kemikali inayoharibu neva huko Salisbury, Uingereza, Machi 2018.

**BBC**



Rais Lazarus Chakwera akiwasalimia wafuasi wake baada ya kuapishwa mjini Lilongwe, Malawi, jana. **PICHA: REUTERS**

# Waziri Mkuu apinga kukamatwa Waziri wa Sheria

**KINSHASA, DRC**

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Sylvestre Ilunga, amepinga kitendo cha kukamatwa kwa Waziri wa Sheria, akisema serikali ya mseto inaweza kuvunjika juu ya suala hilo na kumtaka rais kuwahakikishia mawaziri utetezi wa kisheria.

Waziri wa Sheria, Celestin Tunda, alikamatwa na polisi Jumamosi jioni na kuachiwa baada ya saa kadhaa za kuhojiwa na waendesha mashtaka katika mahakama, kusababisha mgogoro wa kisiasa katika serikali ya mseto iliyoko madarakani.

"Hili suala nyeti na ambalo halijawahi kutokea linaweza kudhoofisha utulivu na utendaji wa mshikamano wa taasisi mbalimbali na kusababisha serikali kuvunjika," alisema Waziri Mkuu Ilunga.

Inadaiwa kuwa Tunda alikwaruzana na Rais Felix Tshisekedi juu ya mabadiliko ya mahakama yaliyopendekezwa na chama cha Tunda, ambayo yataipa Wizara ya Sheria udhibiti zaidi juu ya uendeshaji wa kesi za jinai.

Lakini wanaopinga mabadiliko hayo wanasema yatadumaza uhuru wa mahakama.

Kutokubaliana huko kumeonyesha mvutano uliopo katika serikali ya mseto baina ya Rais Tshisekedi na washirika wa mrithi wake aliyekuwa madarakani kwa muda mrefu, Joseph Kabila.

Kabila aliachia madaraka mwaka jana lakini anaendelea kuwa na madaraka mapana kupitia wawakilishi wake walio wengi bungeni na kuwa wanashikilia wizara nyingi na ofisi ya waziri mkuu. Tunda anasauti katika Chama cha PPRD cha Kabila.


"Hakuna kiongozi wa serikali ambaye anaweza kushtakiwa kwa sababu ya maoni yaliotolewa wakati wa majadiliano ya Baraza la Mawaziri," alisea Ilunga akirejea mkutano wa Ijumaa ambapo Tshisekedi na Tunda walikwaruzana juu ya mabadiliko ya mahakama.

Alisema mahakimu waliohusika katika ukamatwaji wa kikatili na kiholela wa Tunda lazima wachukuliwe hatua za kisheria.

Rais Tshisekedi aliingia madarakani Januari 2019, na kuunda serikali ya mseto kwa kushirikiana na Kabila, lakini muungano huo umeendelea kuonyesha dalili za kukosekana kwa mshikamano.

Maelfu ya waandamanaji walijumuika kupinga sheria hiyo iliyopangwa katika viwanja vya bunge Jumatano. Walitimuliwa na polisi waliotumia mabomu ya kutoa machozi na maji yenye kuruka kwa nguvu.

***RFI***



# FLICK

## HAFIKIRII ALCANTARA KUONDOKA BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

HANSI Flick amesisitiza kwamba hafikiriii Thiago Alcantara anaweza kuondoka Bayern Munich, huku kiungo huyo akiwa anahusishwa na mpango wa kwenda Liverpool.

Thiago mwenye umri wa miaka 29, mkataba wake unamalizika mwakani na mabingwa hao wa Bundesliga, huku mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool wakiripotiwa kutaka kumsajili.

Lakini Flick anataka kumbakiza Thiago, akimtaja mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania kuwa ni "mchezaji wa aina yake".

"Sifikirii kuhusu hili kabisa, kwamba Thiago anaweza kuondoka kwetu," amesema kocha huyo wa Bayern baada ya kuibuka na ushindi wa 4-0 dhidi ya Wolfsburg.

"Mara zote nimesema kwamba, Thiago ni mchezaji wa aina yake ambaye anaweza kuipa timu vitu vingi. Kwa hiyo, sifikirii kuhusu hilo.

"Na nafikiria baada ya mchezo na kumalizika kwa msimu, unatakiwa kukubali kwamba huwezi kujibu kila swali la mwandishi wa habari."

Thiago aliwasili Bayern akitokea Barcelona mwaka 2013, akishinda taji la Bundesliga kila msimu klabuni hapo.

Bayern ilimaliza msimu huu wa Bundesliga kwa kufikisha mabao 100, kwa mabao ya Kingsley Coman, Mickael Cuisance, Robert Lewandowski na Thomas Muller.

# SOLSKJAER ASIFIA KIWANGO CHA MAGUIRE

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amemsifia Harry Maguire "kwa mchango wa aina yake" kwa Manchester United baada ya mlinzi huyo kufunga bao la ushindi dhidi ya Norwich City.

Maguire alifunga bao hilo dakika ya 118 wakati United wakiibuka na ushindi wa 2-1 pale kwenye dimba la Carrow Road Jumamosi na kufuzu nusu fainali ya kombe la FA.

Mlinzi huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 80 kutoka Leicester City mwaka jana, Maguire ameisaidia kuiimarisha United kucheza mechi 14 bila kufungwa katika mashindano yote na Solskjaer alimsifia sana nahodha huyo.

"Harry ni mchezaji wa aina yake tangu amekuja klabuni kwetu," alisema kocha huyo wa United akiwaambia waandishi wa habari.

"Uongozi wake imara umeonekana, ametusaidia kuimarisha timu na nafikiri ameshinda kila changamoto, hivyo nina furaha sana na Harry."

Baada ya Todd Cantwell kusawazisha lile la Odion Ighalo, Norwich walipunguzwa na kubakia wachezaji 10 wakati Timm Klose alipotolewa nje kwa kadi nyekundu dakika ya 89.

Man United waliopo nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi, watacheza na Brighton and Hove Albion Jumanne.



# SETIEN AJITETEA KUMWACHA BENCHI GRIEZMANN

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Quique Setien amesema huwa hachagui mchezaji kwa kuangalia bei ya mchezaji aliyosajiliwa nayo wakati akipanga timu, huku akimwanzisha Antoine Griezmann benchi dhidi ya Celta Vigo.

Griezmann, ambaye alinunuliwa kwa euro milioni 120 kutoka Atletico Madrid mwaka jana, aliingizwa baadaye wakati Barca wakilazimishwa sare ya 2-2 dhidi ya Vigo Jumamosi.

Setien alitetea uamuzi wake wa kutomwanzisha Griezmann, ambaye alifunga mabao 14 katika mechi 42 msimu huu.

"Sifikiri kuhusu bei ya mchezaji ninapomwanzisha mchezaji," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Wiki iliyopita tulichagua kikosi sahihi, na leo nikaanza tofauti. Wiki iliyopita waliniuliza mimi kuhusu Ansu Fati kwamba hachezi, kwanini Riqui Puig hakucheza na leo wanauliza kwanini Griezmann hakuanza.

"Hayo ni maamuzi ninayoyafanya ni maamuzi ya kiufundi. Hivyo nafanya kutokana na namna ninavyouangalia mchezo wenyewe."

Lionel Messi alitengeneza mabao mawili kwa Luis Suarez, lakini Iago Aspas alisawazisha dakika ya 88 na kulazimisha sare na Barca.



## HABARI MICHEZO



# LAMPARD
## AMTAKA PULISIC KUWA KAMA STERLING

**LONDON, England**

FRANK Lampard amemtaka fowadi wa Chelsea, Christian Pulisic, kujiimarisha na kufikia kiwango kama Raheem Sterling, Mohamed Salah na Sadio Mane.

Pulisic alifunga bao la uongozi wakati Chelsea wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Manchester City pale Stamford Bridge, Alhamisi na matokeo yake kuwafanya Salah, Mane na wachezaji wenzao wa Liverpool kubeba taji la Ligi Kuu ya England.

Pulisic, ambaye alinunuliwa kwa pauni milioni 56.7 kutoka Borussia Dortmund, pia alifunga wiki iliyopita wakati wakiibuka na ushindi pale Aston Villa na sasa ana mabao nane katika mashindano yote tangu aanza msimu huu na Blues.

"Nafikiri anaweza kuwa mchezaji mkubwa," alisema Lampard.

"Alianza kupata namba wakati akiwa kijana kule Ujerumani na akahamia kwetu na ni uhamisho mkubwa na tunatarajia atapaa zaidi hasa ikichukuliwa umri wake.

"Hakuna shaka kutokana na ubora wake, unaweza kuliona hilo anaonyesha kutaka sana kuimarika.

"Ukiwaangalia wachezaji wanaomzunguka yeye anaweza kujiimarisha zaidi, ana uwezo wa kuwa kama Raheem Sterling ambaye kwa sasa anafanya makubwa. Pia anaweza kuwa kama Mo Salah au Mane."

## ARTHUR APISHANA NA PJANIC BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa Barcelona, Arthur na wa Juventus, Miralem Pjanic jana Jumapili walitarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya, kwa mujibu wa Sport.

Barcelona watamwachia Arthur kwenda Juventus huku akipishana na Pjanic anayetajwa kutua pale kwa miamba hao wa Katalunya.

Arthur ameigharimu Juventus euro milioni 70, huku Pjanic ada yake inatajwa kuwa ni euro milioni 63.

Miamba hao wa LaLiga na Serie A wamefanikiwa kufikia makubaliano hayo baada ya uvumi wa muda mrefu.

Arthur na Pjanic walitarajiwa kufanyiwa vipimo vyao jana kabla ya kusaini mkataba wa kuzitumikia klabu zao mpya.

Kwa mujibu wa Sport, Arthur alisafiri kwenda nchini Italia akiongozana na madaktari wa Barcelona mjini Turin.

Halafu Arthur atarudi tena Barcelona kumalizia kipindi kilichobaki cha msimu huu na mabingwa hao wa LaLiga, ambao walitoa sare ya kufungana 2-2 na Celta Vigo Jumamosi.

## SAUL ATAKA KIWANGO ZAIDI ATLETICO

**MADRID, Hispania**

SAUL Niguez ameishauri Atletico Madrid kuendelea kuwa kwenye kiwango chao bora, baada ya kuibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Deportivo Alaves kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Jumamosi.

Atletico sasa wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi baada ya kushinda mechi nne mfululizo, wakati Saul na Diego Costa wakifunga kwenye mchezo huo uliopigwa uwanja wa Wanda Metropolitano.

Saul alionekana kufurahia kuwa kwenye orodha ya wafungaji na amewataka Atletico kuendelea kuwa kwenye kiwango wakielekea kuwavaa Barcelona, Jumanne.

"Nina furaha kubwa kufunga bao la kwanza. Kufunga bila mashabiki kunakuwa na hisia tofauti.

"Walicheza kwa kuzuia zaidi na tulikabiliana na wakati mgumu kipindi cha kwanza, lakini tulipata ushindi," alisema kiungo huyo.

"Tulianza kwa kuwa mbele ya 1-0, baadaye wakatuacha na nafasi, na kwa uhakika kabisa ulikuwa mchezo wa aina yake kwa upande wetu.

"Kuna wakati hatukucheza vizuri, lakini tunatakiwa kuendelea kuwa kwenye kiwango chetu cha juu kabisa."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AITAKA ARSENAL KUIIGA LIVERPOOL

●●●Asema ni mfano mzuri kwao, lakini bado wako mbali sana na...

MIKEL Arteta ana matumaini Arsenal inaweza kuitumia Liverpool kama mfano, lakini amebainisha kwamba, kikosi chake bado "kiko mbali sana" na taji la Ligi Kuu ya England.

Liverpool Alhamisi ilitwaa ubingwa wake wa kwanza tangu mwaka 1990, ikiwa imeshinda mechi 28 kati ya 31 za ligi msimu huu.

Arteta, ambaye kikosi chake cha Arsenal kipo nafasi ya tisa, amesema namna Jurgen Klopp alivyoibadilisha Liverpool ni mfano mzuri kwa timu yake kuufuata.

"Ni mfano mkubwa kuchukua mfumo huu na inawezekana kufanya hivyo. Hilo linahitaji kazi kubwa na maamuzi makubwa kwa watu wote," amesema kocha huyo wa Arsenal.

"Kwanza, imani kubwa ni kile unachokifanya kuhakikisha kinafanyika na wote kuonekana mpo upande mmoja.

"Kutoka kwenye kufanya maamuzi sahihi kwenye suala la kusajili wachezaji na falsafa ya klabu na mashabiki pia wanaona kwamba wao ni sehemu ya timu.

"Na wachezaji ambao wamechukuliwa wanatakiwa kujitoa kwa klabu na kutoa ubora wake wote kwa timu.

"Haijalishi unafanya nini. Baada ya hapo unaanza taratibu kutengeneza ubora wake na kwa uhakika hapo ndipo unaweza kuimarika."

Mafanikio ya Liverpool yamekuja miaka minne baada ya kufungwa kwenye fainali ya Ligi ya Europa, huku Arsenal nayo ilifungwa kwenye kwa mashindano hayo katika hatua hiyo mwaka 2019.

Lakini Arteta alikataa kuzilinganisha timu hizo, akisema Arsenal ipo mbali sana kuweza kubeba taji la ligi.

"Kwa wakati huu tuko mbali sana. Msimamo wa Ligi unaonyesha wazi kwamba, kwa sasa tuko mbali tunataka kufikia mafanikio hayo," alisema.

## KWA UFUPI

**DORTMUND YAJIPA MATUMAINI KWA SANCHO**

BORUSSIA Dortmund inaendelea kuwa na matumaini kwamba, winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20 atabakia klabuni hapo, huku wakiwa bado hawajapata ofa yoyote kwa ajili ya mchezaji huyo. ***(Sport Buzzer, via Goal).***

**LIVERPOOL KUTOA OFA KWA KOULIBALY**

BINGWA mpya wa Ligi Kuu ya England, Liverpool inapanga kutoa ofa ya kumsajili mlinzi wa Napoli, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29 raia wa Senegal, katika siku zijazo. ***(Tuttomercato, via Mail)***

**CHELSEA YAMWANIA ONANA**

CHELSEA inapanga kumsajili golikipa wa Ajax na Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 24, kama mrithi wa Kepa Arrizabalaga. Kipa huyo mwenye umri wa miaka 25 raia wa Hispania amekuwa akihusishwa na mpango wa uhamisho wa kwenda Valencia kipindi hiki cha majira ya joto kwa mkopo wa miaka miwili. ***(Marca, via Express)***

**KLOPP BADO AMFIKIRIA SANCHO**

JURGEN Klopp amebainisha kuwa anafikiri Jadon Sancho "angependeza sana" akiwa na jezi ya Liverpool, lakini kocha huyo hafikirii kama uhamisho wake utawezekana kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Bild, via Liverpool Echo)***

**LEVERKUSEN KUMWACHIA HAVERTZ**

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Peter Bosz, amekubali kwamba dili la Kai Havertz kuondoka klabuni hapo litakamilika Agosti, huku Chelsea, Real Madrid na Manchester United ni miongoni mwa klabu zinazoshindana kuwania saini ya fowadi huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 21. ***(Sun)***

**ARSENAL YAJITOSA KWA SZOBOSZLAI**

ARSENAL imeonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa Red Bull Salzburg, Dominik Szoboszlai raia wa Hungaria. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 mwanzo alikuwa akihusishwa na washikabunduki hao wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2019. ***(Sun)***

**RONALDINHO ATAKA KURUDI KUCHEZA**

NYOTA wa Brazil, Ronaldinho mwenye umri wa miaka 40, anataka kutoka kustaafu soka na kurudi kuichezea klabu inayonolewa na Diego Maradona, Gimnasia mara tu atakapomaliza kipindi chake cha kifungo cha nje nchini Paraguay. ***(Mundo Deportivo, via Sun)***

**JUVENTUS KUTOMUUZA RABIOT EPL**

MKURUGENZI wa Juventus, Fabio Paratici amekanusha mpango wa mazungumzo kuhusu kiungo, Adrien Rabiot kwenda Ligi Kuu ya England huku Manchester United, Arsenal na Everton zote zikiwa zinahusishwa kutaka kumsajili raia huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 25. ***(Sky Sports Italia, via Metro)***

**VALLADOLID WAMTAKA RAMIREZ ABAKI**

KLABU ya Real Valladolid inataka kuongeza muda wa mkopo wa Sandro Ramirez hadi mwishoni mwa msimu huu wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, lakini bado hawajafikia makubaliano na Everton kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 raia wa Hispania. ***(Liverpool Echo)***

**SOLSKJAER AENDELEA KUMFIKIRIA SANCHO**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amekataa kuondoa uwezekano wa kumsajili Jadon Sancho wakati dirisha la usajili litakapofunguliwa. ***(Manchester Evening News)***

**CASTAGNE AITAMANI SPURS**

MLINZI wa kulia wa Atalanta raia wa Ubelgiji, Timothy Castagne mwenye umri wa miaka 24, amekubali kwamba, hatakataa nafasi ya kujiunga na Tottenham Hotspur. ***(Teamtalk)***

HABARI MICHEZO

# JKT TANZANIA YAIPA JEURI MBEYA CITY BARA

**Na Somoe Ng'itu, MBEYA**

USHINDI wa mabao 2-0 walioupata Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya JKT Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini hapa juzi, umeipa nguvu mpya timu hiyo iliyopo katika janga la kushuka daraja, imeelezwa.

Mbeya City sasa imefikisha pointi 33 ikiwa imeshuka dimbani mara 32, na hivyo kubakisha mechi sita ili kumaliza msimu wa 2019/20 unaotarajiwa kumalizika Julai 26, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Amri Saidi, alisema anawapongeza vijana wake kwa kufuata vema kikamilifu maelekezo yake ambayo yalizaa matunda katika mchezo huo.

Saidi alisema bado hawajakata tamaa ya kushuka daraja na wamejipanga kuendelea kupambana hadi dakika ya mwisho katika Ligi hiyo ya juu hapa Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema ushindani wa ligi hiyo msimu huu ulikuwa tangu mwanzo na hivyo anaendelea kuwakumbusha wachezaji wake kuongeza umakini.

"Nimefurahi sana kwa ushindi wa jana (juzi), bado yuko kwenye mapambano, hatujakata tamaa, ushindi tuliopata umetusaidia kupata nguvu mpya kwenye vita tunayopigana, tunaamini tutafanikiwa," Saidi alisema.

Naye Kocha wa JKT Tanzania, Abdallah Mohammed "Bares", alisema kikosi chake kilikuwa na wakati mgumu kutoka kwa wapinzani wao ambao walitumia vema makosa waliyofanya wachezaji wake.

"Hatukuwa na siku nzuri, siwezi kuwalaumu wachezaji wangu, wamenipa matokeo mazuri katika mechi kadhaa zilizopita, bado tunaendelea kupambana ili tumalize vema msimu huu," Bares alisema.

Mabao ya Mbeya City katika mchezo huo wa raundi ya 31, yalifungwa na Patson Shigala na Peter Mapunda.



Mchezaji wa timu ya Boma FC, Agrey Ambangile, akiwa ameruka juu kupiga mpira wa kichwa dhidi ya mchezaji wa Pan African, katika mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza, uliopigwa Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uchaguzi TWFA-Mbeya wanukia

**Na Somoe Ng'itu, MBEYA**

CHAMA cha Soka Mkoa wa Mbeya (MREFA), kimeanza maandalizi ya kusimamia uchaguzi wa viongozi wapya wa Chama cha Soka la Wanawake mkoani humo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa MREFA, Elias Mwanjala, alisema tayari maandalizi ya awali yameshafanyika na wanaamini mchakato huo ukikamilika, wataongeza nguvu mpya ya kusimamia ligi za wanawake.

Mwanjala alisema wanataka kuona Mbeya inakuwa na timu zenye nguvu na hatimaye kuwania nafasi ya kucheza Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

"Maandalizi yako katika hatua nzuri, hatutaki kukaa kimya tena, baada ya kukamilisha uchaguzi wao, mtaisikia Mbeya katika mambo mazuri, tunaweza na tuko tayari kuendelea pale tulipoishia," alisema Mwanjala.

Aliongeza bado wanajivunia kuwa na wachezaji kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), ambao walitokea Mbeya na hiyo inathibitisha jiji lao linahitaji kurudi kwenye ushindani kwenye soka la wanawake.

"Mchezaji kama Opa Clement, ni nyota katika kikosi cha Twiga Stars, kwa sasa anaitumikia Simba Queens, ila ni zao la Mbeya, tunamtakia kila la kheri, na tunataka kutoa wachezaji tegemeo zaidi, tunaamini linawezekana," Mwanjala alisema.

Awali TWFA- Mbeya ilikuwa chini ya mwamuzi mstaafu wa soka wa kimataifa aliyekuwa anatambuliwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), Elizabeth Kalinga, ambaye sasa ni kamisaa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Simba Queens, Ruvuma hapatoshi

**Na Somoe Ng'itu, MBEYA**

TIMU ya Simba Queens kutoka Dar es Salaam inatarajia kuwakabili wenyeji Ruvuma Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Majimaji mjini Songea.

Ligi hiyo imerejea tena baada ya kusimama tangu Machi, mwaka huu kutokana na kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' alisema wamejiandaa kupambana katika mchezo huo ambao utakuwa na ushindani kutokana na ubora wa timu zote mbili.

Mgosi alisema amewaandaa wachezaji wake kuwaheshimu wapinzani wao ili watimize malengo yao ya kuondoka na pointi tatu muhimu za kuwaimarisha kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Alisema kikosi chake kiliwasili salama mjini Songea na wako tayari kwa mchezo huo wa kwanza tangu kutokea kwa janga la corona ambalo lilisimamisha ligi na shughuli mbalimbali duniani.

"Tunataka kuanza nao, ndio ni timu nzuri, lakini nakumbuka wanakutana na Simba Queens, malengo yetu ni ubingwa, tunataka kushinda mechi tatu za kwanza za ugenini, hapo tutakuwa tumejiweka pazuri, halafu mikakati itaendelea tukirudi Dar es Salaam," alitamba kiungo huyo wa zamani wa Simba.

## Machomane yawaza ubingwa wa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya kuwa katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, Machomane United imedhamiria kunyakuwa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu kwa kushinda mechi zake zote zilizobakia.

Kauli hiyo ya Machomane United yenye makazi yake Kisiwani Pemba, imekuja baada ya kushinda rufani yake dhidi ya JKU na kupanda kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Mohammed Kombo, alisema wachezaji wake wanahamasa kubwa ya kusaka ushindi na wana matumaini makubwa ya kuunyakuwa ubingwa wa ligi hiyo ambayo haina mdhamini.

Kombo alisema endapo watashinda mechi nane zilizobakia, tayari watakuwa wametimiza malengo yao ya kuuchukua ubingwa na hakuna klabu itakayowazuia.

"Itakuwa ni zawadi kubwa kwa mashabiki wa timu yetu ambao wengi wao wapo Kisiwani Pemba, wachezaji wangu nimewaambia huu ni muda wa kucheza mpira ili kuhakikisha timu yetu inatimiza lengo lake, na hii itawezekana endapo wachezaji watajituma na kusikiliza kile mwalimu anachowaelekeza mazoezini na hata wanaposhuka dimbani," alisema Kombo.

Machomane itashuka dimbani Julai 4, mwaka huu kuwakabili Chipukizi kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba kuanzia saa 10:00 jioni.

Michezo
Jumatatu Juni 29, 2020
Nipashe



Arteta aitaka Arsenal kuiiga Liverpool HABARI UK 22



Wachezaji wa Simba wakiwapungia mikono mashabiki. **PICHA: MAKTABA**

# SIMBA BINGWA RASMI 2019/20

●●●Yafikisha pointi 79 ambazo hazitafikishwa na timu nyingine, kukabidhiwa kikombe cha ubingwa mkoani Lindi kwa...

**Na Somoe Ng'itu, MBEYA**

SIMBA imefanikiwa kutetea ubingwa wake wa Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Prisons katika mchezo wa ligi hiyo, uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa.

Ubingwa huo ni watatu mfululizo baada ya kikosi hicho cha Mbelgiji, Sven Vandenbroeck kufikisha pointi 79 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine, huku zikiwa zimebakia mechi sita msimu huu kumalizika huku Prisons wakifikisha pointi 43.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi inashikiliwa na Yanga yenye pointi 60 na wakishinda mechi zote watafikisha pointi 78 wakati yenyewe itafikisha pointi 77.

Dakika 45 za kipindi cha kwanza zilimalizika kwa kila upande kutofanikiwa kuliona lango la mwenzake, lakini wenyeji wakionekana kutamba zaidi kwenye eneo la kiungo.

Mbali na kiungo kuonyesha uwezo wake, pia Salum Kimenya na Adili Buha walikuwa katika kiwango bora zaidi wakilisumbua lango la Simba mara kwa mara, lakini kipa wa Wekundu wa Msimbazi, Aishi Manula alikuwa makini kuondoa hatari hizo.

Prisons inayonolewa na Mohammed Rishard 'Adolph' walianza kwa kasi katika mchezo huo na ilifanya shambulizi safi kupitia kwa mshambuliaji wake, Jeremiah Juma, lakini Manula aliwahi kusaka na kuwanyima Maafande hao bao la mapema dakika ya kwanza.

Wenyeji hao waliendelea kulisakama lango la Simba kwa kukaribia kufunga dakika ya 10 kupitia kwa Jeremia ambaye mpira wa kichwa aliyeunganisha kona iliyopigwa na Kimenya, kwa mara nyingine Manula akaudaka mpira huo.

Kipa wa Prisons, Jeremiah Kisubi aliinyima Simba bao baada ya kudaka kwa ufundi mpira wa faulo uliopigwa na Ibrahim Ajibu dakika ya 13 wakati krosi iliyopigwa na Kimenya ilikosea kipimo kidogo na kuwafanya Maafande hao kupoteza nafasi hiyo.

Dakika ya 30 Ezekia Mwashilindi alikaribia kuipatia Prisons bao, lakini Tanzania One Manula alipangua shuti hilo huku Kisubi naye alipangua mpira uliopigwa na Gerson Fraga na kuwabana Wekundu wa Msimbazi nafasi hiyo nyingine ya kufunga goli dakika ya 37.

Simba nayo ilianza kwa kasi kipindi cha pili kwa shambulio lililoanzia kwa Meddie Kagere, lakini pasi yake iliyokwenda kwa Miraji Athumani 'Sheva' ilitolewa nje na Kisubi dakika ya 47.

Manula aliwahi kupangua krosi safi iliyopigwa na Mwashilindi iliyokuwa inaelekea langoni moja kwa moja dakika ya 71 na shambulio lingine dakika iliyofuata kupitia kwa Samson Mbangula, lakini safari hii ukaishia mikononi mwa Manula.

Prisons walifanya shambulizi lingine sekunde chache baadaye, lakini Jeremiah alipiga shuti fyongo na kupoteza nafasi nyingine katika mchezo ambao uliohudhuriwa na Naibu Spika, Tulia Ackson.

***Tanzania Prisons;*** kikosi kilikuwa na Jeremiah Kisubi, Michael Ismail, Benjamin Asukile, Vedastus Mwihambi, Nurdin Chona, Jumanne Elfadhilly, Salum Kimenya, Ezekia Mwashilindi, Samsom Mbangula, Jumanne Juma na Adily Buha.

**Simba;** Aishi Manula, Haruna Shamte, Gadiel Michael, Erasto Nyoni, Kennedy Juma, Gerson Fraga, Hassan Dilunga/ Luis Miquissone (dk 67), Mzamiru Yassin, Meddie Kagere, Ibrahim Ajibu/ Clatous Chama (dk 46) na Miraji Athumani 'Sheva'/ John Bocco (dk 80).

**KOMBE KUKABIDHIWA LINDI**

Taarifa za awali zilizopatikana jijini hapa zinasema, Simba itakabidhiwa kikombe cha ubingwa Julai 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa baada ya kumaliza mchezo wa ligi hiyo dhidi ya Namungo FC.

Hata hivyo, Simba itakuwa na mchezo mwingine katika Kanda ya Kusini, Julai 5, mwaka huu dhidi ya Ndanda FC kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona.

## GWAMBINA YAFUNGUKA ITAKAVYOTINGA LIGI KUU

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukata tiketi ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao, Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Novatus Fulgence, amesema atafanya maboresho madogo katika kikosi chake ili kukiimarisha kuelekea ligi hiyo yenye ushindani zaidi.

Gwambina FC iliyokuwa Kundi A katika Ligi Daraja la Kwanza ilifikisha pointi 44 baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Pamba, pointi ambazo hazifikiwi na timu nyingine katika kundi hilo, huku wakibakiwa na mechi mbili mkononi.

Fulgence aliliambia Nipashe kuwa anahitaji usajili wachezaji wapya sita ili kukiimarisha kikosi chake na hataangalia majina katika mchakato wa usajili wake.

Kocha huyo alisema anataka kuwa na kikosi kipana atakapokuwa anapambana kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza huku akieleza timu hiyo haina 'udugu' na klabu nyingine yoyote.

Alisema ana furaha kufanikiwa kutimiza malengo ya timu hiyo kwa wachezaji wake kufuata maelekezo kwa muda mrefu.

"Haya ni mafanikio makubwa kwetu Gwambina, wote tulikuwa katika mstari mmoja, tulijikita kutimiza malengo yetu, tulihakikisha nidhamu inatawala ndani na nje ya uwanja, na hilo nimefanikiwa," alisema Fulgence.

Kocha huyo alisema ana uzoefu na changamoto zilizoko katika Ligi Kuu Bara, hivyo hataki kuona makosa yanayofanywa baadhi ya timu kucheza msimu mmoja na kushuka daraja yajirudie katika timu yake.

"Bora tutumie nguvu katika usajili kuleta wachezaji ambao wataleta ushindani, lakini pia wawe bora ili waje kutusaidia katika mapambano, Gwambina itakuwa tofauti," alisema Fulgence.

Alisema nguvu nyingi zikitumika katika kusajili wachezaji wazuri na bora watakaosaidia timu hiyo kucheza ligi bila ya presha na hofu.

"Usajili wangu nitaongeza kipa, beki, kiungo na mshambuliaji mmoja, kwa sababu nahitaji kila idara iwe na wachezaji wasiopungua watatu wa kutegemewa," alisema Fulgence.

Bado vita ya kupanda daraja moja kwa moja iko katika Kundi B kati ya Dodoma FC na Ihefu ya jijini Mbeya huku klabu nyingine zitakazoshika nafasi ya pili zikisubiri kucheza mtoano na timu za Ligi Kuu Bara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >